

**Mbaroni** madai ya kusafirisha punda nje ya nchi bila kibali

UKURASA 5



**AG** aonya mawakili wa serikali kwenda kortini bila hati idhini

UKURASA 5


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

**Jumapili Mei 26, 2024** • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581688

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US




## Aziz Ki anogesha sherehe

UKURASA 24

# Viongozi waanika vikwazo amani na usalama Afrika

UKURASA 2







Rais Samia Suluhu Hassan ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika (AU), akipokea Tuzo Maalum kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja huo, Moussa Faki Mahamat, wakati wa maadhimisho ya miaka 20 ya Baraza hilo, jijini Dar es Salaam jana. **Picha** (kushoto) ni Rais Samia, akimvalisha Nishani ya Heshima Rais mstaafu Dk. Jakaya Kikwete kwa kutambua mchango wake katika eneo la Amani na Usalama Barani Afrika na (**picha kulia**) ni Rais Samia, akimvalisha Nishani ya Heshima Rais mstaafu wa Nigeria, Olusegun Obasanjo kwa kutambua mchango wake katika eneo la Amani na Usalama Barani Afrika. **PICHA ZOTE: IKULU**

## ACT yakomaa wajumbe wa tume uchaguzi kuachia ngazi

UK. 3

# Haki jinai kitanzi makamanda Polisi



UKURASA 4


**MICHEZO** **FLICK ARITHISHWA MIKOBA YA XAVI** UK.21 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Othman ataka uungwaji mkono kushika madaraka

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Chama cha ACT- Wazalendo, Othman Masoud Othman, amewataka viongozi na wanachama kuwaelimisha wananchi ili waunge mkono harakati za chama hicho zinazolenga dhamira ya kuleta mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi na kusaidia kuleta maendeleo ya kweli Zanzibar.

Othman ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, aliyasema hayo leo Dunga wilaya ya Kati Unguja, alipozungumza na viongozi wa chama hicho wa mikoa ya kichama ya Kati na Kusini Unguja akihitimisha ziara yake ya shukrani kwa wanachama na viongozi kwa kuchaguliwa kushika nafasi hiyo.

Alisema ni muhimu kwa wanachama na viongozi wa chama hicho kukumbushana na kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kukiunga mkono chama kwa dhamira ya kuleta mabadiliko.

Kwa mujibu wa Othman, serikali isiyo na mamlaka iko kwenye hatari ya kushindwa kutimiza majukumu yake kwa wananchi na kwamba chama hicho ndicho pekee kilichojipambanua kutetea haki ya Zanzibar.

Alisema vyanzo muhimu vya mapato kama vile bandari, forodha, mafuta na gesi kikatiba si ya Zanzibar na hivi sasa yanatumika kwa njia ya makubaliano jambo ambalo ni kinyume cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwamba kuna uwezekano wa jambo hilo kutoendelea ikawa hatari kwa Zanzibar na kushindwa kuendesha shughuli zake mbalimbali.

Mwenyekiti huyo alisema kwamba suala hilo la kutumika fedha hizo kama hisani linaweza kusitishwa iwapo hata upande wa Tanzania Bara mamlaka yake yatashikwa na chama kingine nje ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) jambo ambalo linaweza kuiletea madhara makubwa Zanzibar kiuchumi na kimaendeleo.

Alisema ni muhimu kwa wanachama na viongozi wa Chama hicho kujipanga vyema katika kusimamia dhamira ya chama hicho kutetea haki za wazanzibar kwa kuhakikisha kwamba chama kinaungwa mkono na kupata ushindi katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Mwaka ujao .

Aliwaeleza viongozi hao kwamba chama hicho hakina dhamira ya kutaka viti vya ubunge au uwakilishi kwa nia ya kupata madaraka, bali daraja muhimu la kufikia dhamira na malengo ya kuleta mabadiliko ya kweli Zanzibar.

Othman alitawatahadharisha wanachama wa chama hicho kwamba katika kipindi kijacho kuna uwezekano mkubwa wa fedha nyingi kutumika kununuliwa wanachama na viongozi ili kuvuruga malengo ya chama hicho.

Kuhusu Serikali ya Umoja wa Kitaifa, Othman alisema msimamo wa chama hicho uko bayana kwamba kitaendelea kuwapo kwenye serikali hiyo iwapo makubaliano yaliyofikiwa kama msingi muhimu wa serikali hiyo yatatekelezwa na kwamba kama itashindikana, hawaoni sababu ya kuwmo katika serikali.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Chama hicho, Ismal Jussa Ladhu, alisema viongozi wanahitaji kufanya kazi kubwa ya kuhakikisha chama kinaungwa mkono na kuleta mabadiliko ndani ya Zanzibar ikiwa ni pamoja na kuzuia ufisadi na ubadhirifu wa mali ya umma unaofanywa na baadhi ya viongozi waliopewa dhamana ndani ya serikali.

Alisema viongozi hao wa serikali wamekuwa wakikiuka taratibu na sheria za ununuzi zilizowekwa na serikali na kufanya uamuzi kinyume cha sheria kwa dhamira ya kuendeleza ubadhirifu kwa maslahi binafsi jambo ambalo haliwezi kuondoka bila chama hicho kuungwa mkono na kushika madaraka.

Naye Mwanasheria Mkuu wa ACT Wazalendo, ambaye pia ni Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shaaban, aliwataka viongozi wa chama hicho kuhakikisha kwamba wanajenga uwezo wa chama kwa kuwa na mtandao mpana wa wanachama ambao watafanya kazi kubwa ya kukiletea ushindi chama hicho katika uchaguzi ujao.



Vijana wakivusha pikipiki katika Mto Mbwemkuru, unaounganisha wilaya za Ruangwa na Kilwa, mkoani Lindi, ambao daraja lake limekatika kutokana na mvua kubwa zilizonyesha, wakati Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alipotembelea kukagua uharibifu uliotokea, jana. **PICHA: OWM**

# Vikwazo amani, usalama Afrika vyatajwa

**Na Restuta James**

MAPINDUZI ya serikali, uchaguzi usio huru na haki, migogoro ya kivita na ugaidi unaotokana na imani kali katika baadhi ya nchi za Afrika, vimetajwa kuwa vikwazo kwa Afrika huku viongozi walioko madarakani na wastaafu wakitaja mbinu za kuzikabili.

Mambo hayo yaliainishwa jana jijini Dar es Salaam kwenye maadhimisho ya miaka 20 ya Baraza la Usalama na Amani la Afrika (PSC), yaliyohudhuriwa na viongozi waandamizi wa serikali barani Afrika na marais wastaafu na wajumbe wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika (AU).

Katika mkutano huo ambao kaulimbiu inasema: "Miaka 20 ya PSC Kama Chombo cha Kudumu cha Uamuzi Miongo Miwili Ijayo ya Amani na Usalama wa Afrika Tuitakayo", viongozi hao walipata fursa ya kujadili mustakabali wa ulinzi na usalama wa bara hilo.

Mwenyekiti wa Baraza hilo kwa Mei, 2024, Rais Samia Suluhu Hassan, akihutubia mkutano huo, alisema ushirikiano wa pamoja unahitajika kuondoa vikwazo hivyo.

Rais Samia aliwataka viongozi wa Afrika kujihoji sababu za migogoro na watu kuingia madarakani kinyume cha sheria na katiba na kwamba njia pekee ya kuitoa Afrika kwenye vita ni kuheshimu kanuni, sheria na katiba pamoja na uamuzi wa PSC.

"Hatua za awali za kudhibiti migogoro ni muhimu kwa kuwa, hazina gharama kubwa ni lazima kuimarisha uzuiaji wa migogoro, mifumo ya utambuzi wa mapema wa matishio ya vita na kuruhusu majadiliano na maridhiano," alisema.

Rais Samia alishauri kuwa nchi za Afrika zitumie nyenzo na mifumo ya Umoja wa Afrika (AU) na kwamba ni wakati muafaka kuwa na jeshi la utayari na mfuko wa amani wa Afrika.

"Ili kukabiliana na ugaidi, tuwekeze zaidi katika kuimarisha utengamano wa kikanda," alisema.

Samia alisema miongo miwili ya PSC inatoa nafasi kwa viongozi kutafakari namna nchi wanachama wa AU zinavyoweza kushughulikia ugaidi, migogoro na mabadiliko ya serikali yasiyozingatia sheria na katiba.

"Jitihada za pamoja ni muhimu katika kukabiliana na changamoto za kiusalama. Miaka 20 iliyopita wakati baraza hili likianzishwa, lilipewa dhima ya kushughulikia migogoro kwa ufanisi na kuimarisha uwezo wa kuleta amani na usalama barani Afrika kwa kutambua nafasi hasi ya vita na mapigano katika kurudisha nyuma maendeleo ya jamii," alisema Samia.

Alisema baraza hilo limeendelea kusimamia misingi ya haki za binadamu, demokrasia na utawala bora, huku likiangazia ushirikishwaji wa wanawake na vijana kwenye masuala ya amani na usalama.

PSC, alisema inashirikiana na jumuiya za kikanda, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa na Umoja wa Ulaya, hivyo kuongeza ushawishi wa Afrika duniani.

Kuhusu Tanzania, Rais Samia alisema itaendelea kutoa kipaumbele katika kuhakikisha kwamba, AU inafikia malengo iliyojiwekea.

"Historia ya mafanikio yetu katika harakati za ukombozi wa Bara la Afrika lazima itupe hamasa katika jitihada zetu za sasa katika kulinda amani, kujiletea maendeleo na kuhakikisha ustawi wa watu wetu.

"Kaulimbiu ya PSC mwaka huu inatutaka kufanya tathmini ya safari yetu tangu kuanzishwa kwa baraza hili hadi sasa na kutafakari kwa kina tuendako.

"Baada ya miongo miwili ya baraza, tumejifunza nini ,na ni mikakati ipi tunapaswa kuiweka ili kuhakikisha tunakuwa na Afrika tunayoitaka yenye amani katika miongo miwili ijayo," alisema Rais Samia.

Alisema tangu kuanzishwa kwa PSC, limekuwa na nafasi muhimu katika kukuza amani, usalama na utulivu barani Afrika na kwamba, Tanzania ina dhamira ya kukuza na kudumisha amani ya Afrika ili kujenga mazingira rafiki ya kijamii na kiuchumi kwa watu wote.

Awali, Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika, Moussa Faki, alisema miongoni mwa viashiria vya kuvunjika kwa amani barani Afrika ni nchi wanachama kutozingatia matakwa ya kidemokrasia ya kuwa na chaguzi huru na za haki.

Alisema licha ya kuwapo kwa PSC, AU haina uwezo wa kuziwekea vikwazo nchi wanachama zinazokiuka katiba na itifaki za baraza hilo.

Faki ambaye alikuwa Waziri Mkuu wa Chad, alisema kuna haja ya kufanya tathmini kuhusu katiba na itifaki iliyoanzisha baraza hilo kuhusu uchaguzi na demokrasia.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba, alisema Tanzania itaendelea kutoa mchango wake katika kulinda amani na usalama barani Afrika kwa kuchangia vikosi vya kulinda amani vya AU, UN (Umoja wa Mataifa) pamoja na misheni za pamoja za Afrika.

**MARAIS WASTAAFU**

Akizungumza katika mjadala wa marais wastaafuulioratibiwa na Kamishna wa Masuala ya Siasa, Amani na Usalama wa Tume ya Umoja wa Afrika, Balozi Bankole Adeoye, Rais Mstaafu wa Tanzania, Dk. Jakaya Kikwete, alisema kutoheshimu uamuzi wa wananchi kwenye sanduku la kura, ndicho chanzo cha migogoro mingi barani Afrika.

Kikwete aliyekuwa akitoa uzoefu wake katika utatuzi wa migogoro, alisema kutozingatia miongozo ya uchaguzi huru na haki na upungufu wa kiutawala umesababisha baadhi ya wananchi kukosa imani na demokrasia.

"Aliyeshinda hatangazwi na aliyeshindwa anatangazwa kuwa mshindi. Yote ni kwa sababu ya kukosekana kwa usawa, ubaguzi, ukabila na upendeleo," alisema.

Rais Mstaafu Kikwete akiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Rais wa Awamu ya Nne, alishiriki katika utatuzi wa migogoro katika nchi mbalimbali zikiwamo Kenya na Zimbabwe.

Rais mstaafu wa Nigeria, Olusegan Obasanja, alisema uamuzi wa kuundwa kwa PSC ulikuwa muhimu kwa ajili ya amani na usalama wa Afrika.

Alisema ni muhimu nchi za Afrika kutenga rasilimali kwa ajili ya kuliwezesha baraza hilo, ili liweze kuwa na nguvu ya kuamua mambo yake kwa uhuru.

Naye Rais mstaafu wa Burundi, Domitien Ndayizeye, alipongeza kazi ya kutafuta amani nchini mwake iliyofanywa na PSC.

Katika maadhimisho hayo, Kikwete, Obasanja, Ndayizeye na Faki, walipewa nishani ya heshima kwa kutambua michango yao katika eneo la amani na usalama barani Afrika, huku Rais Samia akipewa tuzo maalum kutoka kamisheni ya AU.

Baraza hilo limeridhiwa na nchi wanachama wa AU 53 kati ya nchi wanachama 55.

## HABARI KITAIFA

# ACT yakomaa wajumbe tume uchaguzi kujiuzulu

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha ACT Wazalendo kimezidi kuwataka wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) wajiuzulu na kufanyika mabadiliko madogo ya Katiba kuwaondolea kinga viongozi hao ya kung'ang'ania kupata fursa nyingine katika Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi .

Makamu Mwenyekiti wa Chama hicho Tanzania Bara, Isihaka Mchinjita, aliyasema hayo jana katika mkutano wa hadhara uliofanyika Tanga mjini.

"Hawa ni wajumbe wa tume ambao mikono na nguo zao zimeloa damu na machozi ya watanzania. Wajumbe hawa kuwavika koti linalowaita kuwa ni watu wema ni dhihaka dhidi ya utu na uhuru wa Tanzania," alidai.

Mchinjita alimwomba Rais Samia Suluhu Hassan asimamie wajumbe hao wa tume kujiuzulu na ahakikishe yanafanyika mabadiliko madogo ya katiba ili kuwaondolea kinga ya kung'ang'ania kupata fursa nyingine.

"CCM ni wanufaika wa hujuma ya uchaguzi ya 2020 iliyofanywa chini ya usimamizi wa tume hii. Chini ya wajumbe hawa wa tume, zaidi ya madiwani 800 na wabunge 28 wa CCM (Chama Cha Mapinduzi) walitangazwa kupita bila kupingwa," alisema.

Katika hatua nyingine, kiongozi huyo alisema Tanzania inaendeshwa kwa madeni kwa kile alichokiita kutokana na wizi unaofanywa na viongozi wa serikali ya CCM.

"Ripoti ya CAG (Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali) imeonesha mwaka huu peke yake Sh. trilioni sita zimeibwa, hii ni sawa na asilimia 20 ya kodi tunayokusanya kwa mwaka, alisema.

Alisema wanalipa deni la Sh. trilioni tisa na mishahara Sh. trilioni 14, hivyo miradi ya maendeleo inategemea mikopo.

"Hii maana yake kila Sh. 100 tunayokusanya, Sh. 20 inaibwa, Sh. 31 inalipa deni na Sh. 49 ni mishahara na posho, hivyo kumaliza fedha zote tulizochanga kupitia kodi na shughuli za maendeleo ya wananchi tunategemea mikopo na wahisani ambako huko ndiko ufisadi mkubwa unafanyika," alisema.

Katika mkutano huo, kiongozi huyo alizungumzia pia suala la viwanda akisema baadhi vimekufa na vilivyobinafsishwa vimegeuzwa magofu na vile vikubwa vimekuwa maghala.

"Tanga ilikuwa ni ukanda wa viwanda kwa Tanzania ilikuwa na kiwanda kikubwa cha mbolea , kiwanda cha plastiki (Amboni Plastic) kiwanda cha chuma, viwanda vya sabuni, kiwanda cha mashati ya Gossage na kiwanda cha nguo na kiwanda cha mbao ambavyo vyote vimekufa yamebaki magofu," alisema.

Kuhusu uuzwaji wa kiwanda cha saruji cha Tanga, alidai kwa sasa hakizalishi saruji badala yake kimekuwa sehemu ya kuchukua malighafi kupeleka Dar es Salaam kwa ajili ya uzalishaji.

"Kilimo mkonge ambao ndio zao kuu la biashara mkoa wa Tanga limeonekana kufa taratibu bado hakuna viwanda vya kutosha vya uchakataji wa zao hili.

"Uzalishaji wa mkonge mwaka 2020 ulikuwa ni tani 36,379, mwaka 2021 tani 36,170, mwaka 2022 zilikuwa tani 44,151, mwaka 2023 tani 56,732, taarifa zinaonesha Tanzania mwaka 1970 iliuzwa nje tani 230,000 ikifuatiwa na Brazil na Mexico," alisema.

Alisema kwa sasa Tanzania ni nchi ya pili ya uzalishaji wa katani duniani lakini hakuna mkazo na jitihada za makusudi za kuendelea zao hilo.

Kuhusu Bandari ya Tanga, alisema licha ya kuunganishwa na reli na kuwa karibu na mikoa kadhaa, bado haitumiwi kimkakati kuchangamsha uchumi wa mkoa huo.




## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya **epaper.ippmedia.com** utachagua toleo unalotaka kununua aidha **Nipashe** au **The Guardian** kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza **"subscribe"**
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa **kadi ya benki** malipo kwa **mtandao wa simu** unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa **namba ya simu** unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. **Kwa benki** unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya **www.ippmedia.com** upande wa kulia utaona **"E-Paper"** utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

MAELEKEZO HAKI JINAI

# Kitanzi kwa makamanda wa polisi

**Na Vitus Audax,** MWANZA

NI KITANZI kwa makamanda wa polisi mikoa. Maagizo ya Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Camillus Wambura, kwa makamanda wa polisi mikoa yote kuanza mara moja utekelezaji kwa vitendo maelekezo yaliyotolewa kupitia Tume ya Haki Jinai yanadhihirisha hivyo.

Rekodi zinaonyesha kuwa jeshi hilo limekuwa likilalamikiwa kwa mambo mbalimbali ikiwamo baadhi ya maofisa na askari kujihusisha na vitendo vya rushwa, uporaji, kubambikia kesi raia na ukiukwaji wa sheria. Hayo ni baadhi ya mambo yanayolitia doa jeshi hilo lililopewa dhamana ya kulinda rai na mali zao.

Katika maagizo yake aliyoyatoa juzi wakati wa uvishaji nishani maofisa, wakaguzi na askari wa vyeo mbalimbali katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, IGP Wambura alisema utekelezaji wa mambo hayo, utaanza kutumika kama kipimo cha utendaji kazi wao. Katika kufanya hivyo, Wambura alisema lengo la serikali ni kuliona jeshi hilo linashika nafasi ya kwanza kwa ubora duniani.

Alisema, maelekezo ya jeshi hilo pamoja na serikali ni kuacha kufanya kazi kwa mazoea, kubadilika kiutendaji na kifikra ili kuhakikisha maofisa na askari wanafanya kazi kwa weledi na kufuata misingi ya jeshi.

Katika taarifa na maelekezo kwa haki jinai jeshi hilo limeshindwa kufuata misingi na sheria ya kuundwa kwake, hivyo makamanda wametakiwa kushirikiana kikamilifu na ngazi nyingine kuhakikisha wanafanya mapitio ya mara kwa mara maelekezo ya Tume ya Haki Jinai na kufanyia kazi kwa vitendo.

"Maelekezo hayo yakachambuliwe vyema na kwa kufuata maelekezo ya serikali kwa kuweka sawa mgawanyo wa kazi na kufanya kazi katika mnyororo mmoja kuanzia ngazi ya taifa hadi kituo cha kata, wote tuongee lugha moja," alisema.




IGP Camillius Wambura. **PICHA: MAKTABA**

### MAELEKEZO TUME HAKI JINAI

Ndani ya Jeshi la Polisi kumekuwapo malalamiko ya muda mrefu kutoka kwa wananchi kuhusu vitendo vinavyochafua taswira ya chombo hicho.

Miongoni mwa malalamiko hayo, yaliyoripotiwa katika Tume ya Haki Jinai ni pamoja na jeshi hilo kushindwa kuzuia uhalifu, matumizi ya nguvu kupita kiasi, kubambikia kesi, vitendo vya rushwa , mali za watuhumiwa kupotea vituoni na kuchelewa kufika kwenye maeneo ya matukio.

Hali hiyo, inasababisha wananchi kupoteza imani kwa jeshi hilo na kutokutoa ushirikiano unaotakiwa katika kukabiliana na vitendo vya uhalifu na uvunjifu wa amani.

Kutokana na malalamiko hayo, tume ilitoa mapendekezo na maelekezo yakiwamo Jeshi la Polisi kufanyiwa tathmini ya kina itakayowezesha kuwapo maboresho makubwa na kuundwa upya ili kuondoa kasoro za kiutendaji.

Vilevile, ilipendekezwa jeshi hilo libadilishwe kisheria, kimuundo na kifikra na kuwa Polisi Tanzania (National Police Service) ili kutoa taswira kuwa chombo cha kuwahudumia wananchi, kubadilisha mitaala ya mafunzo na mtazamo wa askari ili kutoka katika dhana ya ujeshi kwenda dhana ya kuhudumia wananchi,

Kadhalika, tume ilitaka liboreshe mfumo wa ndani wa kushughulikia malalamiko ya wananchi na liimarishe huduma za intelijensia ya jinai na polisi jamii kwa kuanzisha programu za kuisogeza zaidi kwenye jamii.

Mambo mengine yaliyopendekezwa ni pamoja na Matumizi ya Amri Kuu za Jeshi la Polisi (PGO) kutokana na kubaini kuwa izmetengenezwa pasipo kuzingatia masharti na wigo wa kisheria uliopo katika kifungu cha 7(2) cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi na sheria nyingine.

Pia ilibainika kuwa miongoni mwa mambo yenye shida kubwa katika PGO ni pamoja na uchunguzi wa vifo vyenye utata, gwaride la utambuzi wa mhalifu, hivyo kutaka PGO yenye GN. Na. 351/2021 inayotumika sasa isitishe matumizi yake na PGO iliyokuwapo awali iendelee kutumika.

### KAULI ZA SAMIA

Tangu alipoingia madarakani machi 19, 2021 Rais Samia Suluhu Hassan amefanya vikao na maofisa wakuu na makamanda wa polisi huku akihimiza jeshui hilo kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria.

Katika kikao cha tathmini ya utendaji kazi kwa mwaka 2020/21, kilichofanyika Agosti 25, 2021 Oysterbay, Dar es Salaam, Rais Samia alilitaka Jeshi la Polisi kutimiza majukumu yake ipasavyo kwa kutenda haki kwa jamii na kuepuka kutumia nguvu kuwakandakiza wananchi.

Aidha, Februari 4, 2022 Rais Samia alikemea matukio ya mauaji ambayo yalikuwa yakiripotiwa, ambayo yalidaiwa kufanywa na baadhi ya askari polisi na kuagiza kuundwa kamati maalum kuchunguza chanzo cha mauaji hayo.

Katika kipindi hicho, kulikuwa na taarifa za mauaji katika mikoa ya Mtwara, Mbeya, Mwanza, Moshi na Dodoma huku baadhi ya maofisa na askari wa jeshi hilo wakitajwa kuhusika.

"Nimemwelekeza Waziri Mkuu aunde kamati nyingine iende ikafanye uchunguzi wa mauaji yaliyofanywa na Jeshi la Polisi alafu watuletee taarifaa. Lakini wakati huo huo, nataka jeshi lijitafakari waone kinachotokea ni kinyume cha misingi ya jeshi la polisi," alisema.

Rais Rais Samia pia aliwataka maofisa wa polisi kuwaacha huru watu ambao wanahisi upelelezi wao hautakamilika katika kesi zao ili wakafaidi uhuru wao wakiwa nje na kama kesi haina mwelekeo, watu hao waachiwe huru lakini kwa zile kesi ambazo wana uhakika upelelezi utatimia, ziharakishwe ili watu wasisote mahabusu.

Sambamba na hilo, aliahidi mbele ya maofisa hao, wakati huo jeshi likiongozwa na IGP Simon Sirro kwamba atafanya mabadiliko. Muda mfupi baadaye, alitekeleza hilo kwa kumteua Wambura kushika nafasi hiyo huku Sirro akipelekwa kuwa Balozi wa Tanzania nchini Zimbabwe. Kabla ya uteuzi huo, Wambura alikuwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI).

### NISHANI ASKARI

IGP Wambura wiki hii, amekuwa akiwavalisha nishani maofisa na askari wav yeo mbalimbali katika kanda mbalimbali huku akibainisha kuwa serikali imeendelea kutambua mchango wa jeshi hilo kwa kuboresha maslahi ya watumishi, kuongeza ajira pamoja na miundombinu.

"Kwa hatua hii ya nishani tunazozitoa pamoja na mambo mengine, Rais Samia Suluhu Hassan ameweka alama isiyofutika katika mioyo ya askari wetu kwa ishara ya kutambua michango na kazi nzuri zinazofanywa na jeshi hili nchini, hivyo tunashukuru saana," alisema.

Wambura pia alisema jeshi hilo lilikuwa na ombwe kubwa la upandishwaji vyeo kwa muda mrefu lakini kwa kipindi hiki Askari wamepandishwa vyeo katika ngazi mbalimbali sambamba na utolewaji wa ajira ambazo zimekuwa zikitolewa kila mara lengo likiwa ni kuongeza nguvu kazi katika jeshi hilo.

Vilevile, alisema maboresho makubwa ya miundombinu mbinu ya jeshi yakiwamo majengo pamoja na ununuzi wa vitendea kazi yakiwemo magari yameendelea kufanyika hivyo kutufanya sisi kama jeshi kuwa na deni kubwa kwa serikali.

Aidha alisema jeshi hilo limedhamilia kuhakikisha linazidi kiimarisha amani na kuwa suala la uvunjifu wa amani haina nafasi katika taifa, hivyo kuahidi kufnya kazi kwa moyo na ushirikiano kutokana na kupatiwa rasilimali za kutosha.

Akizungumza kwa niaba ya askari walipokea nishani, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Naibu Kamishna (DCP) Wilibroad Mutafungwa, alisema nishani hizo zitawaongezea morali, nidhamu na uwajibikaji katika utendaji kazi na kuahidi kuendelea kusimamia na kutekeleza majukumu kwa weledi na misingi ya jeshi hilo.

"Tunaomba hatua hii iwe endelevu kwa kuendelea kutoa nishani hizi kutambua michango, majukumu na uwezo wa askari, hali inayoongeza chachu katika utumishi," alisema DCP Mutafungwa.

# AG aonya mawakili wa serikali kwenda kortini bila hati idhini

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali (AG), Dk. Eliezer Feleshi, ameonya tabia ya baadhi ya mawakili wa serikali kwenda mahakamani bila ya kuwa na hati idhini kutoka kwa, Mwendesha Mashitaka Mkuu Serikali (DPP).

Akifunga mafunzo ya siku tatu kwa mawakili wa serikali jana jijini hapa, Dk. Feleshi alisema ni utovu wa nidhamu kwenda mahakamani, bila kuwa na hati hiyo, kwani wanakuwa hawana maelezo ya kutosha ya mtuhumiwa na kusababisha haki kutotendeka.

"Sitegemei kuona tena hili likirudia wakili wa serikali anapoenda mahakamani kuendesha mashauri ni lazima apewe hati idhini ya kuendesha mashauri," alisema.

Alisema serikali inatarajia mawakili wanapozijua vizuri sheria na miongozo mbalimbali ya kisheria, itaepusha hasara serikali pale inaposhtakiwa na kuepusha migogoro isiyo ya lazima.

"Hivyo kila wakili wa serikali ni lazima ahakikishe anafanya kazi zake kwa kuzingatia weledi na ubora sambamba na kuzingatia miongozo iliyopo ili kutenda haki," alisisitiza.

Dk. Feleshi alisema uwapo wa mafunzo hayo, yatasaidia kuwaongezea uwezo wa kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi ndani na nje ya nchi, ili kuhakikisha serikali inapata uwakilishi bora katika mahakama mbalimbali.

Vilevile aliwasihi mawakili hao kuzifahamu vizuri kanuni za uchaguzi na kutenda haki kipindi cha uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu na Uchaguzi Mkuu mwakani.

"Hatutegemei nyie muwe miongoni mwa kuminywa demokrasia, sisi tuwe miongoni mwa wale wanaomsaidia Rais Samia Hassan Suluhu, katika kusimamia demokrasia na kutenda haki," alisema.

Wakili Mkuu wa Serikali, Dk. Boniphace Luhende, alisema mafunzo hayo yameshirikisha mawakili wa serikali 600, kutoka taasisi mbalimbali za serikali, zikiwamo wizara na Bunge.

Taasisi nyingine ni idara za serikali, mashirika ya umma, wakala wa serikali, mamlaka za udhibiti, halmashauri za majiji, manispaa, Miji na wilaya, Vyuo mbalimbali vya serikali, benki na washiriki kutoka ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

# Mbaroni madai kusafirisha nje punda 46 kinyume cha taratibu

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kikosi cha Kupambana na Kuzuia Wizi wa Mifugo kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi Wilaya ya Longido mkoani Arusha wamekamata watuhumiwa wanne pamoja na punda 46 waliokuwa wakisafirishwa kinyume na taratibu kwenda nje ya nchi.

Kamanda wa Polisi wa Kikosi hicho nchini, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Simon Pasua, alisema watu hao wamekamatwa kwa kushirikiana na wananchi pamoja wizara hiyo.

Kamanda Pasua alisema watuhumiwa hao wanashikiliwa na Jeshi la Polisi, huku majina yao yakihifadhiwa kwa sababu za kiupelelezi.

Alisema tayari serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilishatoa maelekezo kuhusu katazo la kusafirisha punda na mazao yake kutokana na kupungua kwa idadi yao.

SACP Passua aliweka wazi kuwa, jeshi hilo litaendelea kuwakamata wale wote watakaobainika kuhusika na usafirishaji wa wanyama hao kwenda nje ya nchi.



Kamanda wa Polisi Kikosi cha Kuzuia wizi wa Mifugo nchini, SACP Simon Pasua akikagua mifugo aina ya Punda 46, baada ya kuwakamata kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, wilayani Longido, mkoani Arusha jana, waksafirishwa kwenda nje ya nchi kinyume na taratibu, ambapo watuhumiwa wanne wametiwa mbaroni. **PICHA: ABEL PAUL** .

# Miundombinu iliyoathiriwa na mvua sasa kurejeshwa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI mkuu, Kassim Majaliwa amesema serikali imejipanga kuendelea kurejesha miundombinu yote ya barabara zilizoathiriwa na mvua zilizonyesha nchini.

Amesema hayo jana alipokagua daraja lililoko katika kijiji cha Nambilanje ambalo limeharibika kutokana na mafuriko. Daraja hilo linaunganisha wilaya za Liwale na Ruangwa.

"Kwa wakati huu ambao barabara nyingi zimekatika na kuharibiwa na mvua, Si mkoa wa Lindi pekee, eneo hili TANROADS (Wakala wa Barabara Tanzania ) wameshafika, wameangalia hii hali na Waziri wa Ujenzi (Innocent Bashungwa) ameshatoa taarifa kwamba wanaendelea na uhakiki," alisema.

Majaliwa alisema serikali inasubiri taarifa ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kuhusu kuisha kwa mvua ili itoe fedha na kutangaza zabuni za ujenzi za ukarabati na matengenezo ya maeneo yote yaliyoathiriwa.

Aidha, Majaliwa alisema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan anatoa pole kwa Watanzania wote waliopata athari ya mvua hizo.

"Nawasihi muendelee kuwa watulivu na mjenge imani na Serikali yenu Mheshimiwa Rais katika mipango yake nina uhakika daraja litafanya kazi," alisema.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu aligawa pampu 20 na mabomba yatakayotumika kumwagilia kwenye bustani za mboga kwa wakazi wanaojishughulisha na kilimo hicho eneo la Nandagala, Ruangwa mkoani Lindi.

Majaliwa aliwataka wananchi wachangamkie fursa ya kilimo hicho kwani kilimo cha mbogamboga kinawezesha mkulima kupata kipato cha haraka.

"Tunataka eneo hili liwe kituo kikuu cha upatikanaji wa mazao ya mboga," alisema Majaliwa.

Aidha, alisema serikali imeendelea kuweka mikakati endelevu ya kukuza sekta ya kilimo ikiwemo mpango wa kutumia mabonde mbalimbali nchini ikiwemo yaliyo katika wilaya ya Ruangwa kukusanya maji ya mvua na kuyatumia katika kilimo na mifugo.

# MAONI & UCHAMBUZI

**Nipashe**
MWANGA WA JAMII

## Mafanikio ardhi yawe kichocheo kufanikisha vipaumbele kisekta

**WIZARA** ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, juzi iliwasilisha bungeni makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2024/25 ambayo yameainisha miradi mbalimbali itakayotekelezwa na lengo kubwa ni kuongeza ufanisi.

Jerry Silaa, Waziri wa Wizara hiyo, wakati akiwasilisha hotuba ya makadirio hayo, alibainisha kuwa ili kutekeleza majukumu hayo kwa ufanisi, aliomba bunge kuidhinisha Sh. 171,372,508,000.

Fedha hizo, alisema ni kwa ajili ya kutekeleza vipaumbele mbalimbali ikiwamo kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro ya ardhi na kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi. Vingine ni kuimarisha mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utunzaji kumbukumbu, upatikanaji wa taarifa za ardhi, kuhakikisha kunakuwapo na nyumba bora, ukuaji wa sekta ya miliki na kuimarisha mipaka ya kimataifa.

Aidha, alisema katika mwaka unaomalizika, wizara imetekeleza kwa mafanikio masuala mbalimbali ikiwamo utatuzi wa migogoro ya ardhi huku akibainisha kwamba imechukua hatua dhidi ya watumishi waliokengeuka kimaadili wakiwamo 22 waliosimamishwa kazi kupisha uchunguzi wa tuhuma zinazowakabili, huku saba walifukuzwa kazi na wawili wakipewa onyo.

Kuhusu mafanikio, alisema miradi iliyosimama kwa muda mrefu, ukiwamo wa Kawe 711, sasa inaendelezwa. Mradi huo, alisema kwa sasa umefikia asilimia 35 na unatarajiwa kukamilika Aprili, 2026 ukiwa na thamani ya Sh. bilioni 169.

Katika kushughulikia migogoro ya ardhi iliyoonekana kuwa kero kitaifa, alisema wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imetatua migogoro 4,565 kupitia kliniki tembezi za ardhi nchi nzima. Pia alisema wizara imeongezewa bajeti Sh. bilioni 287.66 ili kulipa madeni ya wazabuni, watumishi na makandarasi.

Pia maombi 191 ya ardhi ya uwekezaji mkubwa, eneo la hekta 11,613 yaliidhinishwa katika mwaka wa fedha 2023/24.

Mafanikio mengine ya wizara hiyo, ni yale yanayohusu wawekezaji wa ndani na nje, ambao thamani yake ni Sh. trilioni 1.08.

Licha ya kuainisha mafanikio hayo, uko ushahidi wa wazi kwamba wizara hiyo hivi karibuni imeonyesha dhamira ya dhati katika kutatua kero zilizokuwa zikiharibu taswira yake na serikali kwa ujumla.

Ziara za viongozi, wakiongozwa na Waziri Silaa ni kielelezo tosha cha kuivalia njuga migogoro ya ardhi ambayo imekuwa ikiripotiwa kila uchao.

Hatua iliyofikiwa na wizara katika kutatua kero hizo ndani ya wizara hasa katika halmashauri mbalimbali ambako watumishi wa sekta ya ardhi wamekuwa wakituhumiwa kuhusika na migogoro hiyo ni ya kupigiwa mfano na kupongezwa.

Ni dhahiri kwamba kama moto uliowashwa mwaka wa fedha unaoelekea ukingoni uliwachoma wengi wakiwamo wale waliokuwa wamedhulumu ardhi za wananchi, utaendelea kwa kasi kubwa zaidi katika mwaka ujao wa fedha. Viongozi wanapaswa kufukua zaidi madudu yaliyojificha pamoja na kusimamia vyema mipango ya matumizi ya ardhi ili kuwe na viwango bora kwenye sekta hiyo.

Pamoja na imani hiyo, uongozi wa juu pekee wa wizara hauwezi kutatua migogoro ndani ya sekta hiyo bali zinahitajika nguvu za pamoja baina ya wizara na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na wizara zingine za kisekta. Wizara hizo ni pamoja na zile zenye dhamana ya maliasili na utalii, kilimo na mifugo kwa kuwa shughuli zao zinahusiana moja kwa moja na masuala ya ardhi.

Aidha, uaminifu kwa maofisa waliopewa dhamana ya kusimamia sekta ya ardhi katika ngazi za halmashauri, unahitajika katika kufikia mafanikio malengo yaliyokusudiwa. Pia elimu itolewe kwa viongozi wa vijiji na wananchi kuhusu namna bora ya matumizi ya ardhi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

## Bodaboda acheni haraka kunusuru maisha yenu

**CHANZO** kikuu cha ajali za bodaboda ambazo wakati mwingine husababisha vifo na majeruhi, kinatajwa kuwa ni uharaka walionao madereva na ukosefu wa mafunzo ya usalama barabarani.

Uharaka huo na ukosefu wa mafunzo ya usalama barabarani, unasababisha baadhi yao kutovaa kofia ngumu, kubeba abiria zaidi ya mmoja, kitendo ambacho wakipata ajali huwa rahisi kuumia vichwa na kupoteza maisha.

Lakini pia kuendesha kwa kasi kubwa pikipiki inaweza kumshinda dereva na kujikuta akipata ajali inayoweza kumsababishia kifo na hata abiria wake.

Kwa mantiki hiyo, ingekuwa vyema iwapo madereva wa bodaboda wataacha haraka zinazosababisha wavuke hata kwenye makutano ya barabara bila kuruhusiwa na taa, wavae kofia ngumu ili kunusuru maisha yao.

Mtindo huo wa haraka umekuwa pia ukiwasababishia ajali hata waenda kwa miguu wanaovuka barabara kwenye eneo la pundamilia au kwenye makutano ya barabara ambako kuna taa za kuongozea vyombo vya moto.

Mfano, magari yanaweza kusimama kwenye eneo la alama ya pundamilia na kusimama kupisha waenda kwa miguu wavuke, lakini madereva wa bodaboda huwa hawasimami, kitendo kinachosababisha ajali mara nyingi.

Wanafanya hayo pia katika makutano ya barabara ambako kuna taa za kuongozea vyombo vya moto, wao huwa hawasubiri kuruhusiwa na taa hizo, hupenya na kuvuka upande wa pili wa barabara bila kujali kwamba kuna taa.

Kwa sasa inaelezwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI), Prof. Abel Makubi, kwamba asilimia 60 ya majeruhi wa ajali, hasa bodaboda, wanaumia sehemu za ubongo.

Kwa mujibu wa Prof Makubi, kwa wastani, kwenye idara ya magonjwa ya dharura wanapokea wagonjwa 15 hadi 20 wanaotokana na dharura mbalimbali huku asilimia 60 zinatokana na ajali za bodaboda.

Prof. Makubi anasema madereva wengi wa bodaboda huwa wanaumia mifupa na ubongo. Madereva hao wanajikuta katika matatizo hayo na kusababisha ajali, huku elimu ya usalama barabarani ikitolewa mara kwa mara, kitendo kinachoonyesha kuwa hawaizingatii.

Kwa mtazamo wangu, umefika wakati sasa kwa wadau wa usalama barabarani kuchukua hatua zaidi dhidi ya madereva wa bodaboda wasiozingatia utaratibu, kanuni na sheria ili kuwanusuru wao na abiria wao.

Kama itapendeza basi askari wa kikosi cha usalama barabarani wanaosimama pembeni mwa makutano ya barabara, wawe wanawakamata madereva wote wanaovuka bila kufuata sheria.

Hatua hiyo inaweza kusaidia kupunguza ajali kuliko ilivyo sasa ambapo wanaweza kuvuka upande wa pili wa barabara hata bila kuruhusiwa, na tena bila woga kwamba kuna askari anawaona.

Ikumbukwe kuwa ajali hizo ambazo inaelezwa kuwa nyingi zinasababishwa na kutozingatia sheria ya usalama barabarani, zinapoteza nguvu kazi ya taifa ambayo ni vijana.

Vijana hao wamejiajiri kupitia sekta hiyo bila kuwa na elimu ya sheria za usalama barabarani wakati wakitekeleza majukumu yao ya kila siku. Hivyo, ni vyema wawe tayari kupokea elimu ambayo hutolewa kila mara.

Kwa wale ambao wameshaipata, hawana budi kuizingatia ili waweze kufanya kazi yao kwa ufanisi, badala ya kufanya wanavyotaka, kana kwamba hakuna sheria, kanuni wala utaratibu.

Ni kweli ajali haina kinga, lakini pia ni muhimu kuchukua tahadhari badala ya kuendesha chombo cha moto bila umakini wowote, kitendo ambacho kinaweza kusababisha ajali zisizo za lazima.

Madereva wangethamini ajira hiyo kwa kuendesha bodaboda kwa kuzingatia elimu ambayo wamepata, lakini hata kama hawajaelimishwa, basi wajifunze kwa wenzao ambao wameshapata mafunzo, kwani hatua hiyo itasaidia kuwafanya wawe salama wawapo barabarani.

SAFU

FIKRA MBADALA

# Hii ndiyo dawa ya kero za Muungano, ubaguzi



Pascal Mayalla

KWA wasomaji wapya, wiki iliyopita nilizungumzia kuhusu kauli za kibaguzi za kunyoosheana vidole vya Utanganyika na Uzanzibari kwamba zinasababishwa na ukosefu wa elimu ya uraia. Katika mwendelezo huo, niliahidi leo kumalizia mjadala huu kwa kuangazia chanzo cha ubaguzi huu na suluhisho la kudumu.

Baada ya Muungano, kwa miongo kadhaa, tumekuwa na Muungano wenye maelewano mazuri licha ya kuwapo kwa changamoto kadhaa kwenye kero za Muungano. Hata hivyo, moto wa Utanganyika na Uzanzibari, uliwashwa na kitendo cha Zanzibar kujiunga na Umoja wa Nchi za Kiislamu (OIC), wakati Tanzania imejinasibu ni nchi isiyo na dini.

Wabunge 55 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT), kutokana na kukiukwa huko kwa Katiba waliunda kundi la G-55 na kuidai serikali ya Tanganyika, ili iendelee kuwa haina dini na kuiruhusu serikali ya Zanzibar kuendelea kuwa mwanachama wa OIC.

Bunge lilipitisha Azimio la kuanzisha serikali ya Tanganyika, jambo ambalo lilimwibua Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, kuwakemea wabunge kwa Bunge kukaa kama kamati ya Chama na kuwaeleza mfumo wa serikali tatu si sera ya Chama Cha Mapinduzi (CCM). Hiyo ilisababisha hoja hiyo ya kuundwa serikali ya Tanganyika,kufa kifo cha mende na kuzikwa jumla.

Zanzibar nayo ililazimishwa kujitoa OIC na kuahidiwa serikali ya JMT itajiunga na OIC, kitu ambacho hakikufanyika mpaka leo. Toka wakati huo, wahafidhina wa Zanzibar wakawa na dukuduku la chini chini kuwa Zanzibar haikutendewa haki, hivyo wakaanza vuguvugu za kudai Zanzibar yenye mamlaka zaidi.

Kabla ya hapo, aliyekuwa Rais wa Zanzibar, Aboud Jumbe, alipewa ushauri wa kisheria na aliyekuwa Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Wolfgang Dourado, wakaandaa hati za kisheria kudai Zanzibar yenye mamlaka kamili, taarifa zikafika kunakohusika. Aboud Jumbe akaitwa Dodoma, akaenda kama Rais wa Zanzibar, akarejea kama rais mstaafu na kusindikizwa nyumbani kwake, Mji Mwema mpaka Mungu alipomuita. Dourado aliwekwa mahali salama, taarifa iliyotolewa ilisema kumetokea kuchafuka kwa hali ya hewa ya kisiasa Zanzibar kulikosababisha Jumbe kujiuzulu urais wa Zanzibar.

Baada ya Rais Nyerere kutoka Bara, alifuatiwa na Rais Ali Hassan Mwinyi kutoka Zanzibar, baadaye akaja Benjamin Mkapa kutoka Bara, akitarajiwa anafuatiwa na rais kutoka Zanzibar. Hali haikuwa hivyo, akaingia Rais Jakaya Kikwete, Wazanzibari wakajiona wamesetwa, wakakoleza hoja ya Uzanzibari. Baada ya Rais Kikwete alifuatia Rais John Magufuli kutoka Bara tena, Uzanzibari ukazidi kukolezwa.

Yaliyotokea Machi 17, 2021 kwa Rais wa JMT kuwa ni Samia Suluhu Hassan kutoka Zanzibar, hoja za Utanganyika zikaanza kuibuliwa tena na wanasiasa mufilisi kuanza tena ubaguzi wa kunyoosheana vidole vya Utanganyika na Uzanzibari.

**TANU NA ASP**

Vyama vilivyopigania Uhuru na ukombozi wa Tanganyika na Zanzibar, TANU na Afro Shiraz Party (ASP) vilipoungana mwaka 1977, si wengi katika Tanzania ya sasa walikuwa wamezaliwa. Wengi wamezaliwa, wameikuta CCM, hivyo hawajui kwa nini TANU na ASP viliungana, na viliungana ili iweje?

Mimi nimezaliwa miaka ya 1960, hivyo TANU na ASP zilipoungana, nilikuwa darasa la tatu, kijijini Itonjanda, nikikaa kwa bibi mzaa Baba, Bibi Wakawombwe (Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi) baada ya Baba Mzee Mayalla (RIP) kuhusika na yale mambo fulani ya Mwanza mwaka 1976.

Sababu ya TANU na ASP kuungana ni kuelekea kwenye serikali moja!. Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere, alisema huu muungano wa vyama vya TANU na ASP na kuzaliwa chama kipya, CCM, ni mwanzo wa safari ya kuondoka kwenye serikali mbili, kuelekea kwenye serikali moja. Je, ndoto hii ya Mwalimu Nyerere kwa Tanzania kuwa nchi moja ya JMT yenye serikali moja na rais mmoja, itakuja kutimia?

Watanzania wanahitaji sana kuelimishwa kuhusu huu muungano wetu adimu na adhimu. Tena ni Rais Samia, kiongozi wa kwanza wa juu aliyetoa ruhusa watu waachwe huru kujadili Muungano. Baada ya Muungano, nchi zote mbili zilitoweka, hakuna nchi ya Tanganyika wala Zanzibar, bali Tanzania ni nchi moja ya JMT yenye sehemu mbili, Tanzania Bara iliyokuwa Tanganyika na Tanzania Visiwani au Tanzania Zanzibar iliyokuwa Zanzibar.

**MKANGANYIKO WA KATIBA**

Kama nilivyosema kimataifa Tanzania ni nchi moja ya JMT, hakuna mkanganyiko wowote wa kimataifa kuhusu Tanzania.

hata hivyo, kitaifa kuna mkanganyiko wa katiba kati ya katiba ya JMT na katiba ya Zanzibar.

Kwa mujibu wa katiba ya JMT ya mwaka 1977, Tanzania ni nchi moja ya JMT yenye sehemu mbili, Tanzania Bara na Tanzania Visiwani au Tanzania Zanzibar. Zanzibar si nchi bali ni sehemu ya JMT yenye utawala wake wa ndani.

Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, inaiita Zanzibar ni nchi, moja ya nchi mbili zinazounda JMT!. Kitendo cha katiba ya Zanzibar kuiita Zanzibar ni nchi, kinawakanganya Watanzania kudhani kuwa nchi ya Tanganyika ndiyo pekee iliyokufa lakini Zanzibar ipo na haikufa.

Naomba niwahakikishie Tanzania ni nchi moja ya JMT. Ile nchi inayotajwa na katiba ya Zanzibar, yaani Zanzibar, sii kweli kuwa ni nchi, bali ni jina tu. Hayo mabadiliko ya katiba ya Zanzibar kujiita nchi, kimuungano ni mabadiko batili lakini kwa vile mabadiliko hayo ni kwa ajili ya Zanzibar tu na hayatambuliwi na katiba ya JMT, serikali ya JMT, imeamua kuyapuuza. Lakini kutokana na hizi kelele, tutapuuza mpaka lini? Si bora twende kwenye serikali moja haya yote yaishe?.

Kwa vile Rais Samia anakwenda kutupatia katiba mpya, nashauri hili la mkanganyika wa katiba kati ya katiba ya JMT na Katiba ya Zanzibar, pia lirekebishwe na kwa maoni yangu, dawa pekee ya uhakika na ya kudumu ambayo ni mwarobaini wa kuzimaliza kero zote za Muungano, ni kwenda kwenye serikali moja.

Nimalizie na hili swali, je, Tanzania sasa tumefika wakati wa kutimiza ndoto ya Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere ya uzalendo wa kweli wa JMT wa kwenda kwenye nchi moja, yenye serikali moja na rais mmoja?

**Wasalaam.**
**Pascal Mayalla**
**+255 754 270403**

# Serikali yatoa maelekezo bei kwa nyumba za WHI

**Na Elizabeth Faustine, MWANZA**

SERIKALI imeiagiza Taasisi ya Watumishi Housing Investments (WHI) kufanya marejeo na kukokotoa upya bei ya kuuza nyumba zao zilizoko kijiji cha Isangijo, Kata ya Bukandwe, wilayani Magu, mkoani hapa, ili ziendane na kipato cha watu wa eneo hilo.

Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, alipotembelea mradi huo na alisema msingi mkubwa wa Watumishi Housing ni kujenga nyumba kwa ajili ya watumishi na ili kuendana na msingi huo, bei za kupangisha na kuuza nyumba ziwe rafiki.

Diwani wa Bukandwe, Marco Minzi, awali akidokeza sababu za watu kushindwa kuzichangamkia nyumba hizo ni gharama kuwa juu kulinganisha na hali ya uchumi wa watu wa eneo hilo, hivyo kuomba zipunguzwe.

Minzi alisema nyumba moja yenye vyumba vitatu, sebule, jiko na sehemu ya chakula inauzwa Sh. milioni 82, ambapo ni gharama kulinganisha na watu wa maeneo hayo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Watumishi Housing, Dk. Fred Msemwa, alisema mradi huo ambao ni wa kwanza kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2015/16, ukihusisha ujenzi wa nyumba 59, kwa ajili ya kuziuza kwa watumishi wa umma wa kada zote, mpaka sasa zilizouzwa ni nyumba 20 na 39 zikibaki.



"Mradi huu ulikamilika mwaka 2018. Nyumba 20 zimeuzwa kwa Chuo cha Mipango kilichoko Dodoma ambacho kina kampasi yake hapa Mwanza. Nyumba 39 tumezipangisha kwa watumishi wa umma," alisema.

Hata hivyo, Msemwa alisema wamepokea maombi ya kupunguza bei za nyumba hizo na kuahidi kufanya marejeo ili kukokotoa bei sawa na hali halisi ya kipato cha watu wa hapo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu, Mohamed Ramadhani, alisema bado wana uhitaji mkubwa wa nyumba kwa ajili ya watumishi kulinganisha na idadi ya nyumba zilizoko.

Ramadhani alitaka Watumishi Housing kuongeza nyumba maeneo ya karibu na wanapofanyia kazi watumishi ili kuepusha usumbufu wa kuchelewa ofisini.

"Magu tuna watumishi 3,079, lakini si watumishi wote wana nyumba, kwa hiyo kuna mahitaji makubwa sana ya nyumba kwa ajili ya watumishi.

"Nyumba nyingi zinazopatikana zinaweza kuwa ama zipo mbali na kituo cha kazi au hazina staha na hadhi ya kukaa mtumishi," alisema.

Ramadhani alisema wanatamani kuona miradi kama hiyo inakuwapo maeneo mengine kama makao makuu ya wilaya pamoja na karibu na hospitali ili watumishi wanafanya kazi kwa kupokezana mchana na usiku iwe rahisi kwao.

# Wahitimu SUA wapewa mchongo wa ajira

**Na Christina Haule, MOROGORO**

WAHITIMU wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) wametakiwa kuacha kubweteka bali wachape kazi huku wakitumia ujuzi wa taaluma wanazopata kutatua changamoto za kijamii kwenye kilimo na mifugo.

Mwenyekiti wa Baraza la SUA, Jaji Mkuu Mstaafu Mohamed Chande Othman, alisema hayo juzi kwenye mahafali ya 43 ya chuo hicho yaliyohudhurishwa zaidi ya wahitimu 700 na Mkuu wa Chuo, Jaji Joseph Warioba.

Jaji Chande alisema SUA hufundisha masomo ya sayansi, kilimo na mifugo kwa nadharia na vitendo na kwamba mhitimu akiitumia vizuri nafasi aliyoipata, itamsaidia kupiga hatua katika kukamilisha kusudia lake la kuisaidia jamii kuinuka katika nyanja zote muhimu zikiwamo kilimo na mifugo.

Naye Naibu Makamu Mkuu wa SUA anayeshughulikia Taaluma, Utafiti na Ushauri, Prof. Maulid Mwatawala, aliwataka wahitimu kujenga dhana ya kutosubiri kuajiriwa bali wajiajiri na kutumia ubunifu walio nao katika kutatua changamoto mbalimbali nchini.

Prof. Mwatawala alisema iwapo watatumia ubunifu, watafanikiwa kutoa elimu waliyoipata kwa wahitaji kabla ya kupata ajira, kukabiliana na changamoto zilizopo.

Mmoja wa wahitimu wa chuo hicho, Amina Malongo, aliwashauri wahitimu wenzake kujenga tabia ya kujituma katika utekelezaji wa kazi zao jambo litakalowasadia kufikia malengo ya kilimo.

Alisema mhitimu kupitia elimu aliyoipata, anaweza kujiajiri na kutatua changamoto zinazowakumba wafugaji na wakulima.

Pia alisema kwa kutumia elimu wanaliyoipata wana nafasi ya kujiajiri na kujikita katika mambo mbalimbali muhimu yakiwamo ya ufugaji wa samaki, kilimo na kuendeleza ufugaji na kutatua changamoto za kilimo hasa kwa wakulima wadogo.

Awali, Makamu Mkuu wa SUA, Prof. Raphael Chibunda, alisema chuo kinastahili kujipongeza kwa kuongeza idadi ya nguvu kazi yenye taaluma, ujuzi na weledi kila mwaka ikiwa ni chachu ya kuongeza kasi ya maendeleo nchini.

# Dereva Shabiby mbaroni kwa kusababisha ajali

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

JESHI la Polisi Mkoa wa Morogoro linamshikilia dereva wa basi la kampuni ya Shabiby, Sadick Said, kwa tuhuma za kusababisha ajali katika eneo la Kihonda kwa Chambo, barabara kuu ya Morogoro - Dodoma na kusababisha watu 22 kujeruhiwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Alex Mkama, amethibitisha kukamatwa kwa dereva huyo aliyesababisha ajali wakati akiendesha basi la abiria lenye namba za usajili T. 341 EEU, akitokea Dar es Salaam kwenda Dodoma jana, majira ya saa 12:00 alfajiri.

Basi hilo lilipinduka kutokana na kilichotajwa kuwa ni uzembe wa dereva kukosa umakini barabarani alipojaribu kuipita bajaji iliyokuwa mbele yake na kukutana na bajaji nyingine na katika kujaribu kuikwepa, alishindwa kumudu na basi hilo likapinduka.

Baadhi ya abiria waliokutwa eneo la tukio, Alikwe Masaga na majeruhi Hamis Shaban aliyekutwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, walisema kwa nyakati tofauti walitoka Dar es Salaam majira ya saa 9:00 usiku kabla ya kufikwa na ajali hiyo.

"Tulianza safari alfajiri muda wa saa 9:00 usiku kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma, tukapita salama stendi ya Msamvu Morogoro majira ya sa 12 kasoro asubuhi ambako tulipata mapumziko mafupi na kujisaidia) na kuendelea na safari.

"Tulipofuika Kihonda jirani na daraja la reli ya mwendo kasi, ndipo dereva alitaka liipita bajaji iliyokuwa mbele yake lakini ghafla ilikuja bajaji nyingine ndipo dereva akajaribu kukwepa na kusababisha gari kupinduka, " alisema Masaga.

Ofisa Habari na Uhusiano wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, Beatrice Kapori, alithibitisha kupokea majeruhi 22 wa ajali hiyo ambao wanaendelea na matibabu na mpaka jana mchana walikuwa wanaendelea vizuri.

Naye Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Dharura katika hospitali hiyo, Nafsa Maromba, aliasema kati ya majeruhi hao, 15 ni wanawake na saba ni wanaume na walioumia sana ni watano, wakiwamo watatu waliopata mivunjiko katika maeneo mbalimbali huku wawili wakiumia zaidi maeneo ya mgongo.

Alisema majeruhi wengine wamepata majeraha madogo madogo na michubuko na baadhi yao wamepewa matibabu na kuruhusiwa.

Majeruhi Hamisi Shabani aliyekutwa hospitalini hapo, alibainisha kuumia zaidi maeneo ya mguu na mgongo lakini maumivu yamepungua kidogo na anaendelea na uangalizi wa madaktari.




Basi la Shabiby lenye namba za usajili T. 341 EEU, likiwa limepinduka katika eneo la Kihonda kwa Chambo, barabara kuu ya Morogoro –Dodoma, mkoani Morogoro jana, baada ya kupata ajali na kusababisha watu 22 kujeruhiwa. **PICHA: IDDA MUSHI**

## Ma-DED watakiwa kuondoa tatizo wanafunzi kukaa chini

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, amewaagiza wakurugenzi wa halmashauri za wilaya mkoani hapa kufanya ukaguzi wa haraka kwenye shule za msingi na sekondari ili kubaini uhaba wa madawati na kuondoa tatizo la wanafunzi kujisomea wakiwa wamekaa sakafuni.

Dendego alitoa maagizo hayo jana baada ya kufanya ziara ya kushtukiza katika shule ya Msingi Bomani, iliyoko Manispaa ya Singida, baada ya kusambaa picha mitandaoni zikionesha wanafunzi shuleni hapo wakifanya mitihani yao wakiwa wamekaa chini.

Akizungumza na viongozi pamoja na walimu wa shule hiyo, Dendego alisema picha hizo zilizosambazwa kwenye mitandao ya kijamii zimeleta taharuki kubwa kwa jamii tofauti na hali ilivyo shuleni hapo ambayo ina upungufu wa madawati manane.

Kutokana na tukio hilo, Mkuu wa Wilaya huyo, alionya tabia ya baadhi ya watu kuchukua picha na kusambaza mitandaoni bila kutafuta ukweli, jambo ambalo linapaswa kukomeshwa.

Dendego ametoa siku saba kwa Mkurugenzi wa Manispaa hiyo kuhakikisha anapeleka madawati yanayohitajika shuleni hapo ili wanafunzi waweze kujifunza na kujisomea katika hali bora na nzuri zaidi.

"Serikali imewekeza fedha nyingi katika uboreshaji wa elimu nchini, vitu kama hivi vinapotokea vinaleta mshtuko mkubwa siyo kwa wazazi tu hata kwa jamii nzima kwa ujumla, jambo ambalo halileti picha nzuri na lazima likomeshwe," aliagiza.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Joachim Msechu, alikanusha kuwa shule hiyo haina upungufu mkubwa wa madawati, ni kwamba hawana madawati manane tu na walikuwa kwenye mchakato wa kukarabati madawati mengine yaliyoharibika ili wanafunzi waweze kuyatumia.

Mkuu wa Wilaya ya Singida, Godwin Gondwe, amemhakikishia Mkuu wa Mkoa huo kuwa, maelekezo aliyoyatoa watayafanyia kazi kuanzia sasa ili kuondoa mapungufu madogo madogo yanayotokea katika sekta ya elimu, lengo ni kuimarisha shughuli za ufundishaji wa wanafunzi shuleni yenye watoto 894 na walimu 16

Wiki iliyopita gazeti hili liliripoti wanafunzi 485 wa Shule ya Msingi Kimpungua iliyoko Manispaa ya Singida, wakikakaa chini kutokana na ukosefu wa madawati.

## Mbinu ya kukomesha mikopo kausha damu

**Na Mwandishi Wetu,** MISSENYI

USHIRIKIANO wa wananchi na viongozi wa serikali ndiyo njia pekee itakayowezesha kuwafichua wamiliki wa taasisi za ukopeshaji fedha zisizo rasmi ili watakaobainika hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yao.

Hayo yalisemwa juzi na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi, John Wanga, alipokutana na timu ya wataalamu ya Wizara ya Fedha ambayo inaendelea kutoa elimu ya fedha kwa wananchi wa mkoa wa Kagera katika wilaya za Bukoba, Missenyi, Muleba na Biharamulo.

"Sisi kama viongozi wa serikali tunatakiwa tuendelee kushirikiana na Wananchi kuwakemea watoa huduma wasio na nia njema kwa taifa wanaojali maslahi yao binafsi", alisema Wanga.

Alisema serikali haitasita kuwachukulia hatua watu wote watakaobainika kwenda kinyume cha maelekezo waliyopewa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kabla hawajapatiwa leseni za kuendesha shughuli za utoaji mikopo.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi, Flavian Nturwa, alisema ni wajibu wa waratibu wote wa huduma ndogo za fedha kutoa elimu kwa wananchi katika ngazi zote ili wawe na uelewa mpana wa masuala ya fedha.

"Tutahakikisha tunafanya mikutano ya mara kwa mara kwa wananchi wa pande zote, watoa mikopo na wapokeaji ili wawe na uelewa wa pamoja hususan elimu ya mikataba ili kuepuka kusaini mikataba yenye masharti magumu", alisema Nturwa.

Naye mtoa huduma za mikopo, Salehe Hamisi, alisema elimu itolewe kuhusu utaratibu wa kusajili taasisi za fedha ili Wafanyabiashara waweze kujisajili kwa wingi na kutambulika rasmi.

Ofisa Usimamizi wa Fedha Idara ya Uendelezaji Sekta ya Fedha Wizara ya Fedha, Mary Mihigo, aliwasisitiza wananchi kuwa na nidhamu ya matumizi ya fedha na kutunza akiba.

Wizara ya Fedha inaendelea na utoaji elimu kwa wananchi kuhusu huduma ndogo za fedha ikiwa ni utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha kila mwananchi anafikiwa na elimu ya huduma ndogo za fedha.

# MAISHA

MEI 26, 2024
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili



Ukurasa 14


## Jiachie na gauni la jioni



Ukurasa 15


## MAISHA NI NYUMBA

Zingatia mambo haya unapotafuta eneo la kujenga nyumba



Ukurasa 12

## HARUSI





## TIBU USO KWA NYANYA

Ukurasa 14

# WATOTO

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| C | ■ | C | H | A | M | A |
| H | ■ | ■ | ■ | D | ■ | S |
| A | ■ | T | U | A | ■ | T |
| G | U | U | ■ | B | A | A |
| U | ■ | M | B | U | ■ | A |
| Z | ■ | B | ■ | ■ | ■ | F |
| I | B | A | K | I | ■ | U |


## FUMBO TOTO

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | ■ | | | | | |
| | ■ | ■ | ■ | | ■ | |
| | ■ | | | | ■ | |
| | | | ■ | | | |
| | ■ | | | | ■ | |
| | ■ | | ■ | ■ | ■ | |
| | | | | | ■ | |

Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


BUU, NAE, WAO SAA, SWALA, UJAZO, AGUSE, BONDA, THAWABU, ASTAAFU

## TOA TOFAUTI 5



## AMSHA AKILI


HAYA WATOTO WAZURI, WEKA KIVULI KWENYE KILA NUKTA ILI UJUE NI NANI AMEFICHWA KATIKA MAUMBO HAYA.



## PAKA RANGI



## CHEKA



Alichokifanya daktari

WATOTO wawili walikuwa wakitembea barabarani, mbele walimuona mwendesha pikipiki akihangaika kuwasha.

**Juma:** Habari kaka?

**Mwendesha pikipiki:** Safi tu.

**Juma:**Naona unaangaika na pikipiki tatizo nini?

**Mendesha pikipiki:** Napiga kiki kuwasha

**Juma:** Kwani Aziz Ki anatengeneza Honda?

**Mwendesha pikipiki:** Nyie watoto achene kunitania

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Mimi na mume wangu ndoa iliyeyuka jumla!

***KARIBU tena msomaji wangu tuendelee kuelimishana kuhusu mambo mbalimbali yanayozisibu ndoa nyingi katika jamii yetu. Wiki iliyopita nilielezea sana kuhusu chanzo cha matatizo katika ndoa.***

Leo nigusie baadhi ya roho zinazoangamiza ndoa. Roho za kichawi. Uchawi ni moja ya silaha kubwa ambayo shetani anatumia ili kuwaangamiza wanadamu.

Ni roho inayopindisha hatma ya mtu. Ni roho inayomkandamiza na kumtawala mtu. Roho hii imeleta uharibifu mkubwa sana katika ulimwengu huu tunaoishi. Ndoa nyingi zimevunjika sababu ya uchawi.

Familia nyingi zimesambaratika kwa sababu ya kulogwa na wachawi. Je, unajua nini wachawi wanafanya kuvuruga ndoa na wakati mwingine kuishambaratisha kabisa familia iliyokuwa imetulia?

Wachawi wanaweza kunuiza maneno kinyume cha ndoa yako na kuifanya iharibike. Wanaweza kumuua mumeo au mkeo na wanaweza kugeuza akili ya mkeo au mumeo mkachukiana.

Pia wachawi wanaweza kukupiga giza ili mumeo au mkeo asikuone. Wanaweza kukutupia harufu mbaya ambayo mume wako au mkeo akiinusa inamfanya akuchukie.

> **"Kuna kitovu chenye nguvu kinachomuunganisha kila mwanadamu kwa mababu zake. Hata kama una ufahamu na akili zako, lakini wewe ni matokeo ya mababu zako!**

Nakumbuka binti mmoja umri miaka 19 alikuja kanisani kwa tatizo la kutupiwa harufu mbaya. Anapokuwa peke yake harufu haisikiki lakini akiwa kwenye kusanyiko la watu ndipo huongezeka hadi watu kutaharuki. Anaendelea kuombewa naamini Mungu atamponya na maadui wataaibika.

Roho nyingine sumbufu ni roho za mizimu. Roho hizi ni silaha kubwa sana anayotumia shetani kuwaunganisha watu na kuzimu.

Kuna kitovu chenye nguvu kinachomuunganisha kila mwanadamu kwa mababu zake. Hata kama una ufahamu na akili zako, lakini wewe ni matokeo ya mababu zako!

Uwe unajua au hujui, nguvu za ukoo ulikotoka ndizo zinazoendelea kuathiri hatma na maisha yako. Watu wengi wanateseka sana leo kwa sababu hawajui historia za mababu au ukoo wao.

Nguvu za ukoo kwa asilimia kubwa ndizo zinazochangia kutengeneza na kuathiri hatma yako! Utafiti unaonyesha kuwa maisha ya watu wengi sana yanaongozwa na nguvu za giza kutoka katika koo zao.

Ndoa za watu wengi zimeharibiwa na kuangamizwa na mizimu.Wanawake wengi wanateseka kwenye ndoa zao kwa sababu ya mizimu.

Ipo mizimu kwenye baadhi ya koo zisizoruhusu wanaume kuwa na mke zaidi ya mmoja. Hata kama mwanaume anampenda mke wake kiasi gani, itafanya juu chini kuhakikisha anafanya kosa la kuzini na mwanamke mwingine. Lengo ni kuharibu ndoa yake!

Zipo baadhi ya koo ambazo haziruhusu wanawake kuolewa. Ikitokea kaolewa, mizimu itatengeneza mazingira magumu kwa huyo mwanamke ili tu aachike!

Roho nyingine sumbufu kwa ndoa ni Roho za majini mahaba. Majini haya ni aina ya mapepo yanayoishi baharini (marine spirits). Lengo lao likiwa kuwaunganisha wanadamu na nguvu za giza ili waendelee kutumikia ufalme wa giza pasipo wao kupenda.

Ni kitengo cha shetani kikiwa na lengo kubwa kuharibu na kuua hatma za wanadamu. Ni mapepo mabaya ambayo hushughulika na kuharibu ndoa za watu wengi sana leo.

Wanawake wengi sana wanajikuta wakizini (ngono potofu) na hayo majini kila mara. Ngono potofu ni uwezo wa jini mahaba kupenyeza viungo vyake katika mwili wa mwanamke au mwanaume na kuzini naye pasipo hiari yake!

Hii hufanyika sana kwa waabudu shetani. Wanaacha miili yao inayoonekana ikiwa imelala na kupenyeza roho zao kwa yeyote wanayetaka kuzini naye.

Wanaume na wanawake wengi sana leo wanaamka na kujikuta wamefanya tendo la ndoa na viumbe wasivyovijua pasipo sababu yoyote. Na wakati mwingine hupuuzia na kuhisi kuwa ni ndoto tu, kumbe ni kitu halisi.

Isitoshe, zimekuwepo kesi nyingi sana za haya majini mahaba kuacha fedha za matumizi chini ya mito mara baada ya kuzini na wanadamu. Miaka ya nyuma viumbe hivi vilijulikana kama "popo bawa".

Kadhalika, yamekuwepo matukio ya watu kujikuta wamelala na wafu. Upo wakati haya majini mahaba huwabaka wanawake. Majini haya yana washirika wake.

Hufanya kazi pamoja na makahaba, huvunja ndoa za watu. Haya majini yana majivuno na kiburi kingi. Yanahusika na kutenganisha ndoa za watu, watoto watelekezwe, kutengeneza nguo za kuwashawishi wanaume.

Kwa mfano, nguo fupi na nyepesi zinazoonyesha maungo ya mwili. Pia kupata marafiki wabaya hayo mapepo huwatengeneza.

**Tuishie hapa. Je, una maoni, Kisa? Ujumbe 0715268581.**

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi

# Ni kama tumelala, tumesahau utafiti kustawisha mkonge

KUTOKANA na mabadiliko makubwa ya tabianchi kwa sasa, wakulima wengi wamekuwa wakikosa mavuno kutokana na kutegemea mvua ambazo kwa sasa mtiririko wake si mzuri.

Katika hali hiyo, watafiti wa mkonge wameanza kuhamasisha kilimo cha mkonge kwa wakulima wadogo nchi nzima ili zao hilo litumike kuwaongezea kipato kwa kuwa ni zao linalovumilia ukame. Ni zao ambalo, halina msimu maalumu wa kupanda na halina wakati maalumu wa kuvunwa. Wakati wowote linapokuwa tayari linavunwa.

Kimsingi, zao la mkonge linaweza kuchanganywa na mazao mengine ya msimu kama kunde, mahindi, maharage, alizeti, njegere na karanga kwa vile halina uhaba wa vipando.

Kama bidhaa zitokanazo na mkonge zinaweza kutumika katika tasnia ya kilimo, nishati, ujenzi, famasia, magari, meli, majumbani, ofisini na mazingira mengine, najiuliza kuna utafiti umefanyika ili kubaini mikoa mipya inayoweza kulima au kustawisha mkonge nchini ukiachana na ile ya wakulima wadogo katika wilaya za Muheza, Korogwe, Handeni, Kilosa, Mkinga, Singida, Tarime, Bunda, Rorya, Mkuranga, Rufiji, Ruangwa, Bariadi, Shinyanga na Same?

Kwa nini basi Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB) hadi sasa haijatangaza inafanya utafiti maeneo gani nchini ili kuendelea kuhamasisha kilimo hicho kama ilivyo kwa mazao mengine ya kimkakati ambayo serikali imekuwa ikifanya hivyo?

Kwa nini mashamba ya wakulima wadogo, mashamba yanayomilikiwa na vyama vya ushirika, yasifanyiwe utafiti kama yanafaa kuzalisha mkonge yakatumika kuwafuta machozi Watanzania badala ya kuwaacha wakaendelea kung'ang'ania kulima mazao kama mahindi na wasipate tija katika mavuno?

Hivi agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kuzitaka halmashauri zinazozalisha mkonge, kuanzisha vitalu vya kuzalisha miche bora ya mkonge na kuigawa kwa wakulima ili kufufua mashamba zaidi na kuongeza uzalishaji zao la mkonge nchini limetekelezwa kwa asilimia ngapi?

Nauliza hilo kwa sababu nakumbuka Majaliwa aliwahi kusema mkakati wa serikali ni kuhakikishia wakulima wadogo na wakubwa wanasukumwa kufufua mashamba yao ya mkonge ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo muhimu nchini.

Tunajua mmea wa mkonge unaweza kuishi kwa kipindi cha miaka 10 hadi 25. Kama ndivyo! kwa nini TSB haijaanzisha kampeni ya hamasa kuwaamsha Watanzania kuchangamkia fursa hiyo ya kilimo cha mkonge ili kumhakikishia mkulima kipato cha uhakika?

Taarifa za kitaalam zinaonyesha kuwa mkonge ni zao linalostahimili magonjwa, wadudu na magugu na hata upungufu wa rutuba kwenye udongo. Ni wakati wakati mwafaka sasa serikali kusambaza bure miche ya mkonge kwa wakulima katika mikoa inayofaa kustawisha zao hilo.

Walao Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe ametupa mwanga kwamba serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI-Mlingano) mwaka ujao wa fedha, itaanza ujenzi wa maabara ya kuzalisha miche ya mkonge kwa njia ya chupa. Lakini pia kuna uhifadhi wa mbegu za asili na TARI-Mlingano imeendelea kutunza vinasaba 60 vya mkonge.

Hadi kufikia Aprili, mwaka huu, TSB imesambaza miche milioni 12.6 katika halmashauri 15 nchini. Ni jambo jema kwa kuwa tunalenga kuwainua wakulima wadogo nchini.

Kanzidata ya Wizara ya Kilimo inaonyesha kwa mwaka 2020/21 tani 36,170 za mkonge zilizalishwa nchini, 2021/22 (tani 44.151) na mwaka 2022/23 tani 48,262.99.

Si haba kwa kuwa hadi kufikia Aprili, mwaka huu, uzalishaji wa singa za mkonge umefikia tani 48,262.99 sawa na asilimia 80.4 ya lengo la kuzalisha tani 60,000; na vilevile TSB imetoa mafunzo ya kilimo bora cha mkonge kwa wakulima wadogo 3,952 na wakulima wakubwa 17 ikilinganishwa na lengo la kuwafikia wakulima 8,000.

Ni faraja kusikia, nchi yetu imefanikiwa kuwaunganisha wakulima 2,500 na soko kwa mfumo wa zabuni, ikilinganishwa na lengo la wakulima 2,400 waliokusudiwa; wakati uzalishaji wa mkonge utaongezeka kutoka tani 48,263 mwaka 2022/2023 hadi tani 60,000 mwaka 2023/24.

■ ***Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***

# HARUSI










Imekuwa kumbukumbu nzuri kwa wanandoa Bikela na mkewe Zawadi Kheri, wakati walipofunga ndoa Januari mwaka jana katika msikiti wa Twalha, Mburahati, mkoani Dar es Salaam.

# MITINDO

## Jiachie na gauni la jioni

KUTEMBEA ukiwa na gauni refu la jioni harusi kwa mwendo wa madaha siyo jambo rahisi, kunahitaji uzoefu na kujiamini kwa kiasi kikubwa.

Wanawale wengi wanashindwa kutembea vizuri wakiwa katika vazi hili kutokana na aina ya kitambaa na urefu wake.

Kuna aina ya utembeaji ukivaa gauni la jioni, ni lazima uonekane unapiga hatua nyongefu, huku ikichagizwa na mikatiko inayopendeza.

Haya ni baadhi ya mambo unayotakiwa kuzingatia wakati unataka kuvaa gauni refu la jioni.

**Usitembee** haraka

Chagua gauni ambalo litakufanya utembee kwa madaha, mwendo wa pole na wenye kukupa muonekano mtulivu. Hata kama gauni lako limetengenezwa kwa aina tofauti na sio refu hilo siyo tatizo kwani unaweza kutembea kama inavyohitajika.

**Viatu vinavyokutosha**

Kama unahitaji kuwa huru na raha zaidi katika mwendo, unatakiwa kuvaa viatu vyenye visigino vya wastani. Ni vizuri kujiweka salama zaidi na muonekano mzuri kwa kutovaa viatu virefu kwani vitakufanya uwe mrefu zaidi, hivyo hatua zako hazitapendeza.

**Kiatu kinachoendana**

Hakikisha rangi ya gauni inafanana na kiatu unachovaa ili kuongeza mng'aro na muonekano chanya.

**Jifunze kutembea**

Unatakiwa kujifunza kwa ufasaha kutembea mwendo wa 'kinyonga' ukipiga hatua kwa kuhesabu. Ni muhimu mtu maalum akawa anakuangalia unavyotembea ili kupata mwendo unaotakiwa.

**Kuwa huru, jiachie**

Unatakiwa kutulia, ondoa hofu kuhusu unavyotembea au jinsi ya kusimama. Ona jambo hilo kama rahisi kwako na unaweza kulifanya muda wowote.











UREMBO

# TIBU USO KWA NYANYA





NYANYA ni kiungo muhimu sana kwenye chakula, ina ladha ya kupendeza na kukufanya ufurahie mlo wako.

Hata hivyo, kiungo hiki kina kazi muhimu katika urembo, nayo ni kurudisha ngozi yenye kasoro ikiwamo kuwa na mafuta zaidi.

Kwa kutumia nyanya katika kusafisha uso itakupa matokeo mazuri na yenye kushangaza.

Nyanya inajumuishwa katika huduma ya ngozi ya kila siku kwa kutumia juisi, majimaji au nyanya zilizosokotwa.

Aina zote za ngozi, inatibika kwa chakula hiki chekundu ambacho kinapata umaarufu katika tasnia ya utunzaji wa ngozi.

Wenye ngozi ya mafuta, tumia nyanya uliyokata vipande viwili, anza kusugua uso wako vizuri taratibu na acha kwa muda wa dakika 10 hadi 15 kabla ya kusafisha.

Fanya hivyo mara kwa mara utaupa uso wako kuwa nyororo na kuondoa mafuta yanayoganda na kusababisha chunusi na makovu.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Juisi ya parachichi na maziwa





TUNDA la parachichi limekuwa maarufu kwa matumizi mbalimbali ikiwamo kinywaji cha juisi.

Leo tutazungumzia namna ya kuandaa juisi ya kipekee ya parachichi, ndizi na maziwa.

Hii ni juisi ambayo itakufurahisha na kukupa nguvu kwa siku yako nzima.

**Mahitaji**

Parachichi moja, ndizi moja na maziwa freshi nusu kikombe na sukari kiasi kama utapendelea.

**Jinsi ya kuandaa**

Kata parachichi vipande vidogo na weka kwenye blender, kata ndizi vipande na weka pamoja na parachichi kwenye blenda.

Mimina maziwa kwenye blenda, saga hadi juisi kuwa laini na yenye mchanganyiko mzuri.

Angalia kama juisi ni nzito sana, ikiwa ni hivyo, ongeza maziwa kidogo kufikia kiasi unachotaka.

Mimina juisi kwenye glasi na ukae uionje.

## DONDOO

Na Restuta James

# Kazi za mikono zinavyopamba

USASA wa vitu vingi duniani unahamia kwenye kuboresha vitu vya asili kuanzia aina ya ujenzi wa nyumba hadi mapambo yake.

Leo tunaangazia mapambo ya ndani yanayotokana na vitu asilia kama ukili, katani, migomba na kamba za aina mbalimbali ambazo miongo kadhaa iliyopita zilionekana kama vitu vya watu masikini.

Kama inavyoonekana pichani, ubunifu wa kazi za mikono zilizonakishiwa kwa rangi ni pambo la nyumba za 'matajiri' ndani na nje ya Afrika.

Wataalamu wa mapambo ya ndani wanaeleza kuwa sanaa ya ubunifu ndiyo inayosababisha kazi za mikono kuteka soko la kimataifa la urembo na mapambo.

Anastazia Jonathan, anasema upambaji wa kutumia ubunifu unatokana na vitu vya asili ambavyo havijapitishwa viwandani, unaongeza thamani ndani ya nyumba na kuifanya ya kisasa zaidi.

"Kinacholeta utofauti ni mpangilio wa rangi na uasili unaobakia wakati wa kukamilisha pambo husika...rangi si lazima zipakwe kwenye pambo pekee, unaweza kupaka kadhaa na vingine vikabakia kwa uasili na vikapangwa vizuri ukutani vinapendeza sana," anasema.

Anafafanua kuwa: "Mapambo haya yanafaa ukiweka na kioo lakini ukiyaweka mengi kwenye ukuta mmoja. Ni muhimu sana ukazingatia ukuta unaoonekana zaidi."

Anasema pambo la ukuta linapendeza likiendana na sofa akitolea mfano wa kutumia foronya za batiki kwenye mito ya sebuleni.

Anasema rangi ya ukuta nayo inapaswa kuzingatiwa kabla mtu hajaamua kutumia pambo la asili au batiki.



## MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Zingatia mambo haya unapotafuta eneo la kujenga nyumba

KUMILIKI nyumba iwe ya kuishi au ya kupangisha ili kujiongezea kipato ni moja ya vpaumbele vya mwanadamu. Hiyo yote inaonyesha umuhimu wa nyumba kwa maisha ya kila siku ya mwanadamu kwa kuwa ni jambo muhimu kwa mahitaji ya lazima.

Ili kufikisha azma hiyo, kutafuta ardhi ni hatua ya awali ambayo mtu hufanya katika kuelekea kujenga nyumba ya ndoto yake bila kujalisha mahali alipoipata ardhi hiyo.

Mtaalamu wa ujenzi, Tamiko Hatula, anasema unapochagua eneo la kujenga, yapo baadhi ya mambo ambayo unapaswa kuyazingatia.

Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na kufanya uchunguzi wa historia ya eneo husika unalotaka kununua, kuangalia ufikikaji wake.

"Kiwanja chenye barabara pande zote huhusiana na furaha, afya njema na mafanikio, huwa na hewa, mwanga na nafasi ya kutosha. Kwa kiwanja kisichokuwa na barabara pande zote ni muhimu kuwe na barabara upande wa Kaskazini au Mashariki ili nyumba ikijengwa iwe na mwanga na hewa ya kutosha kuanzia asubuhi," anasema.

Jambo lingine ambalo anashauri kuzingatia wakati wa kutafuta kiwanja kwa ajili ya ujenzi ni pamoja na kuhakikisha eneo unalonunua ni kwa ajili ya makazi au biashara na makazi.

"Hii itakusaidia uepukane na usumbufu wa kubomolewa au kuwa na hofu ya kuhamishwa, hakikisha unafuata taratibu zote za umiliki wa ardhi zilizowekwa," anasisitiza.

Anashauri kuepuka kununua kiwanja kinachouzwa na mtu aliyepatwa na dhiki au kufilisika kwa kuwa baadae kinachangia kukukosesha furaha na amani.

Pia anashauri kuepuka kiwanja kilicho jirani au kinachopakana na maeneo ya mikusanyiko mikubwa ya kijamii ikiwamo kumbi za starehe, kanisa, msikiti, kiwanda, chuo, jeshini, shule, soko, sehemu ya stendi za magari.

"Maeneo haya huwa na kelele nyingi na mara nyingi matumizi yake huathiri maeneo yaliyo jirani,ikiwamo kubadilishwa kwa matumizi wakati wowote na pia ni vigumu kulea watoto na kuwakuza kimaadili katika maeneo hayo," anabainisha.

Mengine anayoshauri kuzingatia ni kuepuka kununua eneo linalomilikiwa au lililomilikiwa na taasisi za kiimani, kuepuka lililo jirani na sehemu ya taka, lenye magofu mengi, mapingamizi, chenye nyufa na mipasuko pamoja na chenye udongo wa mfinyanzi.





## KATUNI



KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
HII NI NINI?
NAONYESHA NNAVYOWEZA KUIKONTROO POMBE!
NASHANGAA MPINZANI WANGU KAKIMBIA BAADA YA KUNIONA! SIJUI KWANINI?
HAJAWAHI KUKUTANA NA ZIRAILI ANA KWA ANA!
LIONE LINADHANI SIFA!
MTANI SIPOI HADI ''NIKUTIE 'KISUKARI'
WALAAAA SIJAKEREKA NA KOMBE LENU
NA SIE TUTALIBEBA KILA MWAKA ILI MSIKEREKE NALO!
'USHABIKI MPAKA MAGETONI NDO NINI MAMA MTU!
BADO UJASEMA

## Mahakama ya kimataifa yaiamuru Israel kuacha kushambulia Rafah

**THE HAGUE,** UHOLANZI

MAHAKAMA ya Kimataifa ya Haki (ICJ) imeiamuru nchi ya Israel kusitisha mara moja mashambulizi ya kijeshi katika mji wa Rafah.

Hukumu hiyo imetolewa juzi jioni kufuatia kesi iliyowasilishwa na Afrika Kusini ikituhumu vikosi vya Israel vinafanya mauaji ya halaiki Ukanda wa Gaza.

Mahakama hiyo ya ICJ yenye makao yake mjini The Hague, nchini Uholanzi imeiamuru Israel kusitisha operesheni za kijeshi huko katika mji huo, ukiwa ni uamuzi wa kihistoria ambao unaweza pia kuongeza shinikizo la kimataifa kwa nchi hiyo kusitisha mapigano.

Jaji Mkuu wa ICJ, Nawaf Salam alisema Israel inapaswa kukomesha mara moja mashambulizi yake ya kijeshi, pamoja na hatua nyingine zozote katika mji wa Rafah, ambavyo vinaweza kusababishia Wapalestina kuishi katika hali ambayo wanaweza kukumbwa na madhila yanayoweza kuwa na athari za kimwili.

" Mahakama inazingatia kuwa kwa wajibu wa sheria za Mkataba dhidi ya Mauaji ya Kimbari, Israel ni lazima isitishe mara moja mashambulizi yake ya kijeshi." alisema

Aidha Mahakama hiyo kuu ya Umoja wa Mataifa imeiamuru pia Israel kufungua mpaka Rafah ili kuhakikisha misaada ya kibinadamu inapatikana na kufikia kiwango kinachokubalika.

Pia mahakama hiyo iliamuru kuachiliwa kwa mateka wa Israel ambao bado wanashikiliwa na kundi la Hamas.

Hata hivyo uamuzi huo wa ICJ huwa ni muhimu kisheria, lakini haina mifumo madhubuti ya kuyatekeleza moja kwa moja hukumu zake. Kwa mfano, iliiamuru Russia isitishe uvamizi wake nchini Ukraine, bila mafanikio yoyote.

Israel ambayo imekuwa ikitetea haki yake ya kujilinda imetoa hoja mbele ya mahakama hiyo kuwa uamuzi unaotaka usitishwaji wa operesheni za kijeshi, ungeliwanufaisha zaidi wanamgambo wa Hamas na kuwazuia wanajeshi wa Israel kuwaokoa watu waliochukuliwa mateka wakati wa shambulio la kikatili la kundi hilo mnamo Oktoba 7 mwaka jana.

Afrika Kusini iliyowasilisha kesi hiyo imeupongeza uamuzi huo na kuzitaka nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa kuunga mkono.

Waziri wa Mambo ya Nje wa nchi hiyo, Naledi Pandor alisema anaamini kuwa uamuzi huu ni madhubuti zaidi katika hatua za muda na unatoa wito uliowazi kukomesha mashambulizi. **DW**

# Ruto afichua muda wowote polisi watapelekwa Haiti

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS wa Kenya, William Ruto amesema kikosi cha polisi kutoka nchini mwake kinatarajiwa kuwasili Haiti kusaidia kuzima ghasia zinazofanywa na magenge ya kihalifu.

Akizungumza na Shirika la Habari la Uingereza (BBC), Rais Ruto alithibitisha ujumbe wa kuandaa kikosi hicho umewasili nchini Haiti na umekutana na kiongozi wa jeshi la polisi wa nchi hiyo ili kuandaa mipango kabla ya wanajeshi hao hawajawasili.

Maoni hayo ya Rais Ruto yalitolewa alipohitimisha ziara yake ya siku tatu nchini Marekani, ikiwa ni kiongozi wa kwanza kuzuru nchi hiyo kiserikali katika zaidi ya miaka 15.

Wakati wa safari yake, Ikulu ya Marekani ilitoa wito wa kupelekwa haraka kwa kikosi cha kimataifa kinachoongozwa na Kenya.

Kauli ya Biden inafuatia wanandoa wa Marekani kutajwa miongoni mwa wamishonari watatu waliouawa nchini humo siku ya Ijumaa.

"Nina timu tayari Haiti ninapozungumza nawe, hiyo itatupa sura ya jinsi mambo yanavyoonekana ardhini, uwezo unaopatikana, miundombinu ambayo imewekwa." Rais Ruto aliiambia BBC juzi.

Aliongeza: "Tunapopata tathmini hiyo tuliyokubaliana na polisi na uongozi wa Haiti, tunaangalia muda wa kati ya wiki tatu na pale kuhusu sisi kuwa tayari kupeleka, itafanyika kila kitu kitakapowekwa tayari. "

Mwaka jana, Kenya ilijitolea kuongoza kikosi cha usalama cha kimataifa kinachoungwa mkono na Umoja wa Mataifa kurejesha hali ya utulivu katika kisiwa hicho cha Caribbean.

Magenge ya kihalifu yamechukua sehemu kubwa ya nchi ya Haiti, na kusababisha vurugu na uharibifu katika mji mkuu wa, Port-au-Prince baada ya mauaji ya Rais Jovenel Moise mnamo Julai, 2021.

Mwishoni mwa wiki hii wamishonari wawili wa Marekani waliuawa nchini humo na wanachama wa magenge hayo.

Akizungumzia matukio hayo, Rais Ruto aliambia BBC kwamba matukio ya aina hii ndiyo sababu nchi yake ilikuwa inajiandaa kupeleka jeshi lake la polisi.

"Hatupaswi kupoteza watu. Hatupaswi kuwa tunapoteza wamisionari, tunafanya hivi ili kuzuia watu zaidi kupoteza maisha kwa magenge." Alisema kwa msisitizo.

Alisema Marekani pia ni sehemu ya muungano wa mataifa mbalimbali ambayo yameamua kufanya kazi na nchi yake kutuliza hali ya hewa Haiti.

Rais Joe Biden aliahidi kuunga mkono kupelekwa haraka jeshi la polisi wakati akizungumza na Rais Ruto. **BBC**



Mwanajeshi wa Israel akijiandaa kufyatua risasi katika mji wa Rafah jana. **PICHA: IDF.**

# Mauaji ya kimbari yahofiwa Darfur

**DARFUR,** SUDAN

JIMBO la Darfur nchini Sudan linakabiliwa na hatari ya kugubikwa na mauaji ya halaiki, wakati ulimwengu ukitilia mkazo mgogoro wa Ukraine na Ukanda wa Gaza.

Angalizo hilo limetolewa na mtaalamu wa Umoja wa Mataifa Alice Wairimu Nderitu, ambaye ni mshauri maalum wa Umoja wa Mataifa wa Kuzuia mauaji ya Kimbari.

"Tuna mazingira ambayo mauaji ya halaiki yanaweza kutokea au yametokea," alisema Nderitu wakati akihojiwa na kipindi cha Newsday cha BBC.

Alisema raia wengi walilengwa kulingana na kabila lao katika mji unaozingirwa na wanamgambo wa RSF wa El Fasher nchini Sudan.

Nderitu, alisema mapigano makali yameongezeka katika siku za hivi karibuni na zaidi ya vifo 700 vimeripotiwa katika siku 10 na shirika la matibabu katika jiji hilo.

El Fasher ni kituo kikuu cha mwisho cha katika eneo la Darfur ambacho kimesalia mikononi mwa jeshi la Sudan.

Wanajeshi walikuwa wakipigana na Wanajeshi wa Rapid Support Forces (RSF) kwa zaidi ya mwaka mmoja, katika vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyosababisha vifo vya maelfu ya watu na kuwalazimisha mamilioni ya watu kuyahama makazi yao.

Mkazi wa eneo hilo Ibrahim al-Tayeb al-Faki, aliiambia BBC dada yake aliuawa katika shambulio la anga la kijeshi ambalo pia liliharibu nyumba yake.

Mwanaume huyo mwenye umri wa miaka 47 aliiambia BBC kuwa alikuwa amewapeleka watoto wake watatu kuishi na babu yao lakini nyumba yao pia ilishambuliwa.

Alisema familia sasa inajificha katika magofu yake ya nyumba hiyo.

"Hakuna mahali salama katika El Fasher hivi sasa," alisema. **BBC**

## MAKALA

# KURASA ZA VIONGOZI KUGEUKA KUWA VYOMBO VYA HABARI



Na Magabilo Masambu

NI kweli kwamba tuna uhuru wa kupashana habari kwa maana ya kutoa na kupokea habari bila kujali mipaka ya nchi. Hii ni kwa mujibu wa Katiba yetu ya nchi. Si dhambi au kosa kisheria kupeana taarifa kwa kuwa dunia imehamia kiganjani.

Leo nizungumzie kuhusu kurasa za mitandaoni za baadhi ya viongozi, hasa wa serikali kugeuka kuwa vyombo kamili vya habari, vinavyohusika kutoa habari rasmi za serikali. Tutakumbuka baada tu ya kuhama katika mfumo wa analojia na kwenda kidijitali, ofisi na taasisi nyingi ziliingia katika mifumo rasmi ya mawasiliano kwa maana ya vitengo vya mawasiliano ambavyo vinamiliki kurasa za mitandaoni.

Katika kongamano la Jumuiya ya Wanahabari wa Mitandao ya Kijamii Tanzania lililoandaliwa na JUMIKITA, lililofanyika katika ukumbi wa Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Mei 21, mwaka huu, na mgeni rasmi akiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, kuliibuka hoja ya baadhi ya viongozi wa serikali kutumia makundi ya WhatsApp kuwasiliana na umma. Hatua hiyo imesababisha waandishi wa habari kukosa fursa ya kuuliza maswali na kupata ufafanuzi wa baadhi ya mambo, hivyo badala yake habari hizo kwenda moja kwa moja kwa umma.

Hoja yangu hapa ni kwamba kurasa za viongozi kutumika kuhabarisha wananchi na kuacha kutumia vyombo rasmi vya kiserikali pamoja na waandishi wa habari ni kudhoofisha vitengo hivyo na tasinia ya habari nchini. Ukweli ni kwamba mitandao ya kijamii ina watu wengi, hivyo habari zitasambaa mapema. Lakini kwa nini kiongozi ndiye aposti habari badala ya kitengo cha mawasiliano? Unakuta kitengo cha habari kwenye taasisi kinamiliki mitandao hiyo ya kijamii kama vile facebook, Twitter, Instagram na WhatsApp lakini baadhi ya viongozi hawatumii kurasa hizo na badala yake wao ndio hugeuka kuwa wanahabari.

Kichekesho zaidi ni kwamba unakuta kiongozi ndiye aliyepakia hayo maudhui au habari, anawahabarisha wananchi halafu anatumia nafsi ya pili! Mfano, Magabilo Masambu ndiye Mkuu wa Wilaya ya Ubungo (Inshallah), anaandika habari yeye kisha anasema Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Mhe. Magabilo Masambu, akizindua mradi wa maji wilayani hapo, amewataka wananchi kutunza vyanzo vya maji! Sasa si useme nikizindua mradi wa maji maana wewe ndiwe uliyezindua, uliyeandika na ndiye uliyeposti.

Hatari nyingine ya jambo hili, tukiachana na kudhoofisha vitengo vya Habari, tutakuwa na habari ambazo hazina ladha ya kiuandishi na kuzifanya ziwe za upande mmoja pekee. Maadili ya uandishi wa habari yanataka habari iwe na mlingano, yaani kiongozi amesema nini na maoni ya wananchi ni yapi. Jambo la pili, je, wananchi wawafuatilie viongozi kwenye kurasa zao au waende kwenye kurasa za vitengo? Kwa mtindo huu, kurasa za kiofisi zinashindwa kukua kwa sababu tunakuwa tunawachanganya walaji namna ya kufuatilia habari.

Jambo lingine, ukiweka mambo ya ofisi kwenye kurasa binafsi, kuna wakati wasomaji wanaonyesha hasira zao kwa sababu kila mtu ana mtazamo wake katika kila jambo. Wengine wanatuka sasa wakitukana kiongozi na wewe unarudishia, unaanza kupambana nao mwisho wa siku atakayeonekana hana maana ni wewe unayebishana naye. Maana wanasema kichaa akikuta umevua nguo unaoga, akachukua nguo, akakimbia nazo halafu na wewe ukamkimbiza, utaonekana kichaa zaidi. Yeye atakuwa anakimbia huku amevaa nguo wakati wewe huna. Najua tunakimbizana kuposti ili waliotupatia dhamana waone ni sawa lakini waone kule kwenye vyombo rasmi haya mambo ya kushindana kujionyesha yanavunja miiko ya taaluma zingine.

Ushauri wangu ni huu, kwa sababu zile kurasa zetu ni za binafsi maana yake tuweke mambo binafsi, umeenda kwenye harusi unataka watu wajuwe ulipiga ubwabwa tupia pale. Umevaa suti nzuri unataka tujue ulikoshona tupa hapo, una mke au mme mzuri unataka jamii imwone bandika hapo, lakini mambo rasmi ya ofisi. Kwa maoni yangu, nadhani yasalie kuwekwa katika kurasa rasmi za serikali na kuwatumia waandishi wa habari tusiwakwepe, ndiyo ajira yao hiyo.

Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumelinda heshima ya wanahabari, tumeviheshimisha vitengo vyetu vya mawasiliano kwa umma zaidi wananchi watakuwa wanapata habari si taarifa. Pili, nashauri Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), iwasajili hao viongozi wanaotumia kurasa zao binafsi kuhabarisha umma kama vyombo rasmi vya habari na walipe kodi, ili tunapotaja kwamba tuna vyombo vya habari vingapi na wao wawamo.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Dar es Salaam-Tanzania**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Jamaa aliyelazimishwa kumrithi mjane wa marehemu kaka yake



Na Adam Fungamwango

INGAWA mambo haya kwa miaka ya sasa yanapungua kwa kasi sana, bado yapo katika jamii, si ya Kitanzania, bali Afrika nzima.

Mambo hayo ni ya kurithisha wajane. Mume akifariki dunia basi ndugu mmoja analazimika kumchukua mjane na kuwa mkewe. Sababu kubwa ilitajwa kuwa ni kulinda mali ya marehemu kwa kuwa mwanamke akikataa kurithiwa, anaambiwa aondoke kwenye 'mji' huo.

Wanawake wengi wakati huo walikuwa hawana chaguo bali kukubali kurithiwa na ndugu ili kuendelea kushi pale alipopazoea na watoto wake.

Kifupi ni kwamba wanawake wakati huo walikuwa zaidi mama wa nyumbani, hawakuwa na kazi yoyote na kama biashara, hivyo zilikuwa zile ndogo ndogo tu za kununua vitu vidogo kama chumvi, kibiriti, mafuta ya taa, sukari na kucheza upatu tu.

Mwanamume anayemrithi mke wa marehemu, awe ameoa au hajaoa, jukumu analopewa ni kuitunza familia ya kaka yake au mdogo wake pamoja na mali zake kama nyumba, mashamba, mifugo, mke na watoto.

Kifupi hapo yeye anakuwa mrithi wa kila kitu, kuanzia mke, na mali zote.

Kila miaka inavyozidi kusonga mbele, haya mambo yanaanza kupungua, nadhani kutokana na elimu, pamoja na maradhi ya UKIMWI. Wako walioendeleza mila hiyo bila kujua kama ndugu kafariki dunia kutokana na UKIMWI, nao wakapata maambukizi na kupoteza maisha.

Kutokana na hali hiyo, ugonjwa huo umesababisa mila ya kurithishana wajane ipungue sana kwani watu wamekuwa waoga, baada ya wengi kuteketea.

Kabla ya hapo, mtu alikuwa hajui ndugu yake amefariki dunia na ugonjwa gani, anamchukua mkewe naye baada ya miaka kadhaa anafariki dunia, anachukuliwa na mwingine, naye anakwenda na maji.

Baadaye watu walikuja kushtuka kinachowamaliza ni Ukimwi, na sababu kubwa ni kurithishana wajane. Pili ni elimu, kwa sasa watu wameelimika, ambapo hakuna mtu anayetaka kutafutiwa mwenza wake na ndugu au wazazi. Kila mmoja anatafuta mwenyewe anayempenda, likimtokea la kumtokea, hilo la kwake sasa.

Kutokana na kukithiri sana kwa tabia hiyo hasa miaka ya nyuma, kama nilivyosema utamaduni huu bado upo, lakini kwa kiasi kidogo sana kwa sasa, bendi ya OTTU Jazz, wana Msondo Ngoma, ilitunga kibao kiitwacho 'Queen Kasse', kuelezea madhila ya jambo hilo.

Ulitungwa na mwanamuziki, TX Moshi William, na kurekodiwa mwaka 1989, likiwa ni tukio la ukweli kabisa lililotokea mkoani Mbeya.

Wakiwa ziarani Mbeya, Moshi alikutana na dada mmoja aliyejiita Queen Kasekenya, ambaye alikuwa ni mmoja na mashabiki wa bendi ya Msondo.

Pamoja na mambo mengine ya stori za hapa na pale, alimuelezea kisa cha hicho ambacho kama kawaida ya wanamuziki wa zamani, ukimweleza mkasa au kitu kinachovutia, atakitungia wimbo tu.

Waliporejea Dar es Salaam, Moshi aliuandika mkasa huo na kutengeneza wimbo ambao akauita kwa jina la yule aliyempa kisa hicho, Kasekenya. Nadhani kisanii na kimuziki, akalifupisha jina la mwanadada huyo na akauita 'Queen Kasse.'

Mashairi wa wimbo huo unaeleza jinsi mwanaume anavyowalalamika wazazi wake kwa kumtaka arithi mke wa kaka yake wakati yeye hataki kufanya hivyo.

Jamaa anasema ana mwanamke anayempenda ambaye ni Queen Kasse, hawezi kumwacha na sababu ya mke wa marehemu kaka yake.

Hata hivyo kwa kuwaridhisha, akawaahidi atamtunza mke na watoto wake, lakini hatomrithi kama mkewe.

"Kaka yako kafariki, chonde mtoto wetu, mke wa watoto, utarithi wewe, ili ukoo wetu usipotee." Wazazi wanamuamuru kijana wao, naye anajibu.

"Ooh! Baba na mama mnisikilize kwanza, kwa haya mnisikilize kwanza, kwa haya nitakayosema, naomba mnikubalie. Kurithi ndoa ya kaka kwangu mimi ni vigumu, na kumuacha Queen Kasse, ni vigumu pia." Kijana anawajibu, na baada ya hapo anawapoza.

"Sikatai ombi lenu bali ninajishauri, kumuacha Queen Kasse, kwangu mimi ni muhali.

"Maneno mliyosema enyi wazee wangu, mimi nimeshindwa, ooh jamani eee, Queen amejaa, rohoni mama, Queen amejaa, rohoni mama aa." Wazazi walipoambiwa hivyo na wao wakaja na hii.

"Kwa hayo uliyosema, wazazi tumesikia, lakini kumbuka kwamba shemejiyo wa watoto, ukumbusho wetu wa marehemu kama yako." Kijana naye anawaahidi kuwatunza, lakini siyo kuwa naye kama mke.

"Naahidi mbele yenu watoto nitawatunza, na hata mama yao Shaddy, simtupi kamwe, lakini Kasse , Kasse, Kasse niko naye, lakini Queen Kasse eee, niko naye.

Sikatai ombi lenu bali ninajishauri, kumuacha Queen Kasse, kwangu mimi ni muhali."

Waafrika, Watanzania, tuendelee kupiga vita moja ya mila potofu ya kurithi wajane.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

KIJANA Heri alikutana na msichana Nuru katika duka fulani maeneo ya Chanika, Dar es Salaam. Baada ya kuongea waliyoongea wakakubaliana kuonana siku ya Jumapili kwenye nyumba ambayo alimuelekeza aje kuulizia. Siku ilifika kama walivyoahidiana, masaa machache kabla ya kuwasili Heri alianza kusikia harufu mbaya chumbani kwake, ambayo kwa uzoefu wake aligundua ni ya panya aliyekufa. Akafanya kila kitu ambacho alidhani kinaweza kinaweza kumaliza tatizo kwani muda ulivyozidi kusonga mbele ndiyo harufu nayo ilizidi. Muda wa Nuru kufika ulikaribia. Njia mbadala aliyotumia kuondoa harufu ndiyo iliyoleta balaa zaidi.

# Harufu ya Panya-9

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Dakika tano zilipita, ndipo Nuru alipoonekana kupatwa na fahamu. Akainuka. Akawatazama watu wawili waliokuwa mbele yake. Akashangaa kidogo, lakini akatabasamu, huku akionekana na aibu.

"Pole mama." Mzee Raia alimpa mkono. Heri hakuonekana kusema chochote. Alikuwa akimtazama Nuru na huruma, iliyochanganyikana na woga pia.

Alikuwa akiwaza kuwa kumbe kitendo chochote ambacho angefanya na Nuru ilikuwa apate matatizo makubwa ambayo yangepoteza maisha ya wote wawili.

Nuru akaitikia kwa kichwa. "Endelea kupumzika, ndani mle nimeona kama kuna mswala hivi, lete ili bibie akalie apumzike, halafu nitazungumza naye baadaye."

Baada ya kuuleta na kumweka apumzike hapo, akamwambia aende dukani kumnunulia chupa ya maji, kwani katika hali aliyokuwa nayo, ni wazi amepoteza maji mengi.

Alichukua dakika mbili mpaka kurejea kwani duka halikuwa mbali sana na hapo.

"Sasa rafiki yangu, njoo ndani nikwambie kitu gani kimesababisha hadi binti huyu amekuwa katika hali hii, na kiumbe gani kilikuwa kinazungumza kwa sauti iliyotoka kwenye kinywa chake."

*******************************

"Huyu binti ana maruhani." Mzee Raia akamwambia Heri baada ya kuingia chumbani.

Walikuwa amesimama wote wawili. Heri alihisi kitu kama hicho hapo awali.

"Alikuwa amepandisha mashetani, na ile sauti iliyokuwa anaongea siyo yake. Ni ya jini ambalo analo. Kwanza nikwambie tu, asingepandisha. Ila hii harufu iliyomo ndani ndiyo imemfanya jini huyo kuja ghafla kichwani mwake, akapandisha. Nadhani ni harufu ya udi ninayoisikia, ni kweli imechoma udi humu?"

"Ndiyo mzee, ni harufu ya udi, niliichoma kwa sababu ndani mwangu kulikuwa na Harufu ya Panya."

"Basi hilo ndilo kosa lako kubwa ulilolifanya, hii harufu ya udi imemfanya huyu binti kupandisha, kwa nini hukumtafuta huyo panya aliyekufa na kwenda kumtupa nje?"




**"Ndiyo mzee, ni harufu ya udi, niliichoma kwa sababu ndani mwangu kulikuwa na Harufu ya Panya."**

"Mzee, yaani nilimtafuta kila kona ya hii nyuma, sikumpata, na muda wa msichana huyu kufika ukawa imeshawadia. Unajua ni aibu sana kwa msichana ambaye kwa mara ya kwanza babu kuja nyumbani kwako, halafu anakutana na harufu ambayo haielewiki, ndiyo maana baada ya kushindwa kumpata, nilikwenda kununua udi ili niondoe harufu kali ya panya."

"Sawa, basi zima kwanza, maana naona bado udi wako unawaka." Mzee Raia alimuomba Heri, na haraka akaenda kuuchomoa alipouchomeka awali, akauzima.

"Hapo sasa sawa. Huyu msichana kilichomsababishia hayo yote huo udi, aliposikia tu harufu akapandishwa na jini lake likaja juu, nadhani umemsikia."

"Nashukuru sana mzee, yaani bila wewe sijui ingekuwaje!" Heri akamshukuru mzee Raia kwa kile alichokifanya, kuzima tukio baya ambalo limemtokea na lingine ambalo lingeweza kutokea pia.

"Mzee nimesikia alipopandisha, jini sijui shetani, limesema tungefanya kitendo chochote lingetukatakata na kunywa damu zetu, ni kweli? Maana imeniogopesha sana!"

"Ndiyo, kuna ukweli kiasi fulani. Mimi kidogo nina ujuzi kidogo na mambo haya, kama asingepandisha maruhani, mngeendelea na starehe zenu kama kawaida, tatizo ni lile lile tu, kuchoma udi ambao umemshtua huko alikokuwa."

"Sasa kwa nini limesema vile?"

"Enhee, umeuliza swali zuri. Yule jini anaitwa Anzura, hili likishamuingia mtu kazi yake inakuwa ni kumzuia mtu kuoa au kuolewa. Wewe unakuwa ni mali yake tu, utatembea kote, utamaliza wote, lakini kwa mwanaume hawezi kuoa, na mwanamke hawezi kuolewa.

Yaani hata kama mwanaume atapanga kuoa, lakini kitatokea kitu chochote tu ambacho kitasababisha ndoa usifungwe, na msichana anaweza hata kuchumbiwa, wakati mwingine hata tarehe ya harusi kupangwa, ila ndugu yangu, haiwezi kufanyika kamwe, kitakachosababisha ivunjike wala hamuwezi kukijua, lakini anakuwa ni huyo huyo jini Anzura.

Nikwambie tu isingekuwa udi ule, mngeendelea tu na mapenzi yenu tu miaka na miaka, lakini kama ungetaka kumuoa, ingeshindikana, tatizo lolote lingetokea." Mzee Raia alisema huku akimkazia macho Heri, ambaye alionekana kushangazwa na mzee huyo kujua mambo mengi yanayohusiana na kilichotokea. Akaendelea kujipongeza kwa kwenda kumwita mtu sahihi.

"Unajua mzee mimi nilikuwa nasikia sana watu anapandisha maruhani, lakini nilikuwa sijawahi kuona hii ndiyo mara ya kwanza. Lakini mbona nasikia kila anayepandisha, jini anakuja na amri au maagizo tofauti tofauti, kwani huwa ni yule yule mmoja au?"

"Hapana." Akajibu mzee Raia na akaendalea. "Majini ni viumbe pia, wako wengi, lakini havionekani kwa macho, na wana uwezo wa kujigeuza kwa taswira mbalimbali, wana uwezo pia wa kumuingia binadamu na kukaa ndani yake kwa sababu mbalimbali, wana majina na kila mmoja ana tabia yake tofauti. Mfano tu nitakutajia wachache, kuna Subiyani, hili kazi yake ni kusababisha ajali, na kunyonya damu za watu, sehemu ambayo linapenda kukaa ndiyo zile ambazo ajali kutokea mara kwa mara. Kuna Makata, hiki linasababisha vifo kwa watu mbalimbali, na binadamu hulitumia kwa kulipiza kisasi kwa alichotendewa na mhusika." Mzee Raia alimwambia Heri ambaye aliendelea kushangaa kwa kile anachoambiwa.

"Kuna lingine linaitwa Subha, hili jini likimpata au kumuingia mtu linasababisha kuwa na kiburi sana na kujikweza, Maulan, likiwaingia watu linawafanya kuwa vichaa, Abuni, linamfanya mtu kuwa na hasira, Al Tarik, lenyewe linapoteza watu katika mazingira ya kutatanisha, Zaitun, lenyewe linasababisha wasichana kuwa na maringo, na Shamsu, hili huvaa umbile la binadamu kwa sura yoyote na majini haya ndiyo yale ambayo huwatokea wanaume wengi kwa umbile la msichana mrembo mno. Yapo mengi sana, lakini kwa uchache ni haya mjukuu wangu, cha kufanya sasa ni moja tu, kumsaidia mwenzako."

"Tunamwokoaje sasa mzee?"

"Yaani hapo cha kufanya ni kuongea naye, ili tufanye utaratibu wa kumtoa mdudu huyu, atamtesa sana kwenye maisha yake. Hatoolewa kwenye maisha yake, hata kama wewe baadaye ukiamua kutaka kumuoa, huwezi."

"Unajua mimi naogopa sana mzee Raia hata kuendelea naye!"

"Hapana kijana, kama nilivyokwambia, yule jini alipanda kwa sababu ya ile harufu ya udi, kwa hiyo tahadhari kama utaendelea naye usiwashe kitu chochote kinachoitwa udi chumbani kwao, au manukato makali siku anapokuja. Au wenyewe mwenyewe usipake pafyumu yenye harufu inayofanana na udi. Hii itakusaidia sana. Ila kikubwa zaidi tumsaidie huyu dada, sasa kwanza tumuulize, halafu tujue la kufanya."

Heri aliona ni jambo jema kwa sababu kama Nuru atakubali hilo, akasaidiwa na kupona, hata yeye mwenyewe itampa sifa kwake na familia ya msichana huyo.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# SHAKIB HANA BAYA

MUME wa mjasiriamali, Zari Hassan, Shakib Lutaaya, ameonyesha jinsi gani anavyoishi kwa furaha na watoto wake wa kambo na kuhisi wapo na baba yao mzazi.

Katika ukurasa wake wa Instagram, Shakib amechapisha video fupi ikumuonyesha Latifah Dangote, akicheza na baba yake huyo nyakati za asubuhi na kumfanyia mizaha ya kitoto.

Tiffah alionekana akinyata kuelekea kwenye kitanda alicholala baba yake kumwekea mikono taratibu wakati Shakib akiwa amelala.

"Wakati umelala lakini Latifah ana mipango mingine.." Shakib ameandika.

# RINGTON HATAKI WANAODANGA

MWANAMUZIKI maarufu kutoka Kenya, Ringtone, amesema amefanikiwa kuwa na ukwasi wa fedha kutokana na kutokuwa na tabia kuwahonga wanawake.

Amesema, kabla ya kuwa mwimbaji alikuwa akifanya biashara ya kuuza CD za muziki na filamu, kazi ambayo ilimpatia pesa nyingi.

Amesema kipindi hicho wanawake wengi hawakumfuata, lakini alipoanza kuinuka na jina lake kuwa maarufu walianza kumsumbua kwa nia ya kutaka pesa.

Hata hivyo,aliwapuuza na kitendo hicho kilimfanya kufanikiwa kutokana na pesa zake kutotumika vibaya kuwapa wanawake wasio na mapenzi ya kweli.



## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**MCKENNA AISUBIRI UNITED**

KOCHA wa Ipswich Town, Kieran McKenna, ambaye amekuwa akihusishwa na Brighton na Chelsea, atasubiri klabu ya zamani ya Manchester United, ambako aliwahi kufanya kazi kama mkufunzi, kabla ya kuamua uhamisho wake mwingine. (**Time**)

**TEN HAG KUONDOKA UNITED**

KLABU ya Manchester United itamfuta kazi, Erik ten Hag, bila kujali matokeo ya fainali ya Kombe la FA dhidi ya Manchester City. (**Guardian**)

**POCHETTINO KUBAKIA EPL**

MAURICIO Pochettino angependa kusalia katika Ligi Kuu England baada ya kuondoka Chelsea na huenda akavutiwa na kazi ya Manchester United ikiwa wataachana na Erik Ten Hag. (**Standard**)

**MARESCA ATAJWA CHELSEA**

CHELSEA inatarajiwa kufanya mazungumzo na Kocha wa Leicester City, Enzo Maresca, wakati wakiendelea na harakati zao za kutafuta mrithi wa Mauricio Pochettino. (**Standard**)

**LEICESTER YAMBANA ENZO**

KIPENGELE cha kuachiliwa kwa Enzo Maresca katika mkataba wake na Leicester kinaaminika kuwa takribani pauni milioni 7.5. (**Talksport**)

**ZEBRI ANUKIA CHELSEA**

CHELSEA haijaondoa uwezekano wa kumnunua Roberto de Zerbi, ambaye aliondoka Brighton kwa makubaliano mwishoni mwa msimu huu. (**Telegraph**)

**BEI YA SANCHO JUU**

BORUSSIA Dortmund inatarajia kufanya mazungumzo kuhusu kubadilisha mkataba wa mkopo wa winga wa Manchester United, Jadon Sancho, ili kuwa wa kudumu baada ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini uwezekano wa kumnunua nyota huyo mwenye umri wa miaka 24 hauonekani kutokana na bei ya klabu hiyo ya Old Trafford kuwa juu sana. (**Sky Sports** )

**KOMPANY, BAYERN KITAELEWEKA**

KLABU ya Bayern Munich itampa Kocha wa Burnley, Vincent Kompany, mkataba hadi mwaka 2027 ili kuwa kocha wao mpya, huku timu hiyo ya Ujerumani ikiwa katika awamu ya mwisho ya mazungumzo na kuhusu kumwajiri Mbelgiji huyo. (**Sky Sports** )

**PIERO ANOGEWA ATALANTA**

GIAN Piero Gasperini anakaribia kusaini mkataba mpya na Atalanta baada ya kushinda Ligi ya Europa. (**L'Eco**)

**SALAH, BRUYNE WASUBIRIWA**

KLABU za Saudi Arabia ziko tayari kusubiri hadi msimu ujao wa joto kujaribu kumsajili mshambuliaji wa Liverpool kutoka Misri, Mohamed Salah, mwenye umri was miaka 31, na kiungo wa kati wa Manchester City, Kevin de Bruyne (32), kwa uhamisho wa bure ikiwa hawatawapata wawili hao msimu huu. (**Telegraph**)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# FLICK ARITHISHWA MIKOBA YA XAVI

## ●●● Ni baada ya Barca kutangaza rasmi imeachana na Xavi ambaye...

**BARCELONA,** Hispania

XAVI Hernández ataacha nafasi yake kama Kocha wa Barcelona baada ya mechi ya leo ya mwisho ya msimu, klabu hiyo ilisema katika taarifa yake.

Chanzo kimoja kiliiambia ESPN Kocha wa zamani wa Bayern Munich na Ujerumani, Hansi Flick, yuko tayari kuchukua nafasi yake.

Rais wa Barcelona, Joan Laporta, alikutana na Xavi baada ya mazoezi ya Ijumaa ili kuthibitisha uamuzi wa klabu hiyo kuhusu mabadiliko ya mwelekeo.

Hatua hiyo imekuja ikiwa ni mwezi mmoja tu baada ya Xavi na Laporta kutangaza katika kikao cha pamoja na wanahabari kocha huyo raia wa Katalunya atatimiza mkataba wake utakaodumu hadi 2025, licha ya kuwa hapo awali alipanga kuachia ngazi msimu huu wa joto.

"Rais wa Barcelona, Joan Laporta amewasiliana na Xavi Hernández hataendelea kuwa kocha kwa msimu wa 2024-25," Barcelona ilisema katika taarifa.

> **"Mkutano ulifanyika kwenye uwanja wa mazoezi mbele ya makamu wa rais Rafa Yuste, wakurugenzi wa michezo Deco na wasaidizi wa Xavi, Óscar Hernández na Sergio Alegre.**

"Barcelona inataka kumshukuru Xavi kwa kazi yake kama kocha, ambayo inaongeza maisha yake yasiyoweza kulinganishwa kama mchezaji na nahodha wa kikosi cha kwanza, na inamtakia kila la heri katika siku zijazo.

"Xavi atasimamia mchezo wa Jumapili dhidi ya Sevilla ambayo itakuwa mechi yake ya mwisho kama kocha.

"Katika siku zijazo, Barcelona itafichua muundo mpya wa ufundishaji kwa wafanyakazi wa kikosi cha kwanza."

Flick mwenye umri wa miaka 59, amekuwa hana kazi tangu alipoacha kazi ya Ujerumani mwaka 2023 lakini amevutia uongozi wa Barca katika mazungumzo, huku ESPN ikiripoti wiki hii kuwa ameibuka kama mgombeaji mkuu kuchukua nafasi ya Xavi.

Kocha wa Barca B, Rafa Márquez na Mkufunzi wa Bayern Munich anayeondoka, Thomas Tuchel pia walizingatiwa, lakini chanzo kilisema mazungumzo na kambi ya Flick sasa yamesonga mbele.

# HENRY ATABIRIWA MAKUBWA



**PARIS,** Ufaransa

KIPA wa zamani wa Ufaransa, Fabian Barthez, amesema, Thierry Henry, amepanga kutwaa medali ya dhahabu katika Michezo ya Olimpiki itakayofanyika kuanzia Julai 26 hadi Agosti 11, mwaka huu jijini, Paris.

Henry ambaye alikuwa sehemu ya kikosi cha Ufaransa wakati kikitwaa Ubingwa wa Kombe la Dunia mwaka 1998, ana jukumu la kuhakikisha timu hiyo inapambana na kutwaa Medali ya Michezo ya Olimpiki.

Barthez ambaye alikuwa sehemu ya mafanikio ya mwaka 1998 amesema anaamini Henry ana nafasi kubwa ya kufanya maajabu katika michuano hiyo, huku akitarajia ushirikiano kutoka kwa watu mbalimbali wa Ufaransa.

"Bila shaka watu wanamtarajia Henry kutwaa medali ya dhahabu ya Olimpiki. Binafsi ninaamini anakwenda kufanya jambo kubwa sana katika Michuano hiyo, kwa hivyo sina wasiwasi naye. Nina ukaribu mkubwa na Henry, na ninamtakia kila la kheri na ninamatumaini atafanikiwa," alisema Barthez.

"Ni Michuano ya Olimpiki, kwa hivyo ni tukio la kimataifa. Tunapaswa kujivunia cha kwetu kwanza, kwa kuamini kinakwenda kufanya maajabu makubwa, ndio maana nimemtanguliza rafiki yangu Henry kwa kuamini anaweza.

Pia ninawatakia kila la kheri wanamichezo wote watakaoiwakilisha Ufaransa katika michezo hiyo, kwa hakika ninaamini wamejiandaa vizuri kwa lengo la kuiletea sifa nchi yetu ambayo ndio mwenyeji." amesema Barthez.

# Ten Hag: Sina uhakika kubaki



**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag amefichua tayari amefanya mazungumzo na mmiliki mwenza wa Manchester United, Sir Jim Ratcliffe, na ataenda likizo siku moja baada ya mechi ya fainali ya Kombe la FA.

Ten Hag alisema uhakikisho kutoka kwa Ratcliffe kuhusu nafasi yake "sio lazima" na akasisitiza alikuwa akipanga "kwenda kwa msimu ujao."

Vyanzo vimeiambia ESPN wakuu wa United wanakagua idadi ya watu wanaoweza kuchukua nafasi ya Ten Hag akiwamo Thomas Tuchel, Mauricio Pochettino, Kieran McKenna na Thomas Frank.

Vyanzo vilivyo karibu na United vimeiambia ESPN wakuu wa vilabu "watapitia msimu baada ya fainali ya FA ya jana."

Lakini alipoulizwa katika mkutano wa wanahabari juzi kama atakuwa sehemu ya ukaguzi wa mwisho wa msimu kufuatia fainali ya kombe hilo, Ten Hag alisema tayari amezungumza na Ratcliffe na uongozi wa INEOS.

"Tayari tumefanya na Jumapili nitaenda likizo, nadhani ninastahili," alisema Ten Hag.

Alipoulizwa iwapo alipewa hakikisho wakati wa mazungumzo kuhusu nafasi yake iko salama kabla ya msimu ujao, Mholanzi huyo alijibu: "Sio lazima, tutakwenda kwa msimu ujao."

## AC Milan, Pioli wamalizana

**MILAN,** Italia

KLABU ya AC Milan imethibitisha itaachana na Kocha, Stefano Pioli aliyedumu klabuni hapo kwa miaka mitano, itakapofika mwishoni mwa msimu huu 2023/24.

Pioli mwenye umri wa miaka 58 ataondoka klabuni hapo huku akiacha kumbukumbu mbaya ya kupoteza mchezo wa Ligi Kuu Italia maarufu Serie A dhidi ya Torino iliyochomoza na ushindi wa 3-1 wiki iliyopita.

Matokeo hayo yameendelea kuwa mabaya kwa miamba hiyo ya mjini Milan, imepata ushindi mara moja pekee katika michezo minane iliyopita kwenye michuano yote, ikipoteza mara nne.

Taarifa iliyothibitisha kuondoka kwa Pioli imeeleza: "AC Milan na Stefano Pioli wamefikia makubaliano ya kuvunja mkataba, kocha ataondoka baada ya kumalizika kwa msimu huu, tunashukuru kwa kufanya kazi na Pioli ambaye alijiunga nasi Oktoba mwaka, 2019.

"AC Milan inatoa shukrani za dhati kwa Stefano Pioli na wafanyakazi wake wote kwa kukiongoza kikosi cha kwanza katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, kutwaa taji la Ligi lisilosahaulika na kuanzisha tena uwepo thabiti wa AC Milan katika michuano mikubwa Barani Ulaya.

"Ustadi wa Stefano na mguso wa kibinadamu umechangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa kikosi chetu, ikijumuisha maadili ya msingi ya klabu tangu siku ya kwanza alipoanza kufanya kazi hiyo.

Pioli amesaliwa na mchezo mmoja wa Ligi Kuu Italia, ingawa Rossoneri watamaliza katika nafasi ya pili bila kujali matokeo ya mechi dhidi ya Salernitana ambayo tayari imeshashuka daraja.



## HABARI MICHEZO

# BIASHARA UNITED, MBEYA KWANZA VITA MUHIMU LEO

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Mbeya Kwanza inatarajia kuivaa Biashara United leo katika mechi ya marudiano ya kusaka tiketi ya kurejea Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona mkoani, Mtwara.

Katika mechi ya mkondo wa kwanza, Mbeya Kwanza ilipata kipigo cha mabao 2-0 kutoka kwa Biashara United, mchezo uliopigwa Mei 19, mwaka huu kwenye Uwanja wa Karume Musoma mkoani, Mara.

Ili kuvuka hatua hiyo, Mbeya Kwanza itakazimika kushinda kuanzia mabao 3-0 na kuendelea ili kuingia hatua inayofuata kwa ajili ya kuzisubiri timu zitakazomaliza nafasi ya 13 na 14 kutoka kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mshindi kati ya timu hizo mbili, Biashara United au Mbeya Kwanza ambazo zilishuka daraja kutoka Ligi Kuu msimu mmoja wa 2021/22, anaweza kurejea tena pale atakapopata ushindi dhidi ya timu moja kati ya mbili zitakazotoana katika mechi za 'play off.'

Timu hizo zimelazikika kucheza mchujo, baada ya kumaliza nafasi ya tatu na ya nne katika Ligi ya Championship msimu uliomalizika kwa KenGold kutangazwa mabingwa wapya.

**Mbeya Kwanza ilimaliza nafasi ya tatu ikiwa na pointi zake 65, Biashara United ikiwa na nne, ilikusanya pointi 62, huku ikiziacha KenGold na Pamba zikipanda Ligi Kuu moja kwa moja.**

Msimu uliopita, Mashujaa FC ya Kigoma ilipanda Ligi Kuu kwa kushinda mechi yake ya 'play off' dhidi ya Mbeya City ambayo ililazimika kucheza mchezo huo, baada ya kufungwa na KMC katika michezo miwili ya mchujo, nyumbani na ugenini.

Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajiwa kumalizika keshokutwa, hivyo timu zitakazoshuka daraja moja kwa moja na zile zinazosubiriwa kucheza mechi za mtoano zitajulikana baada ya pazi la ligi hiyo kufungwa rasmi.

Tayari Yanga imeshatangazwa kuwa mabingwa wapya wa msimu huu wa 2023/2024.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya vijana wa umri chini ya miaka 15 wakishangilia baada ya kutwaa ubingwa wa mashindano ya African Schools Football yaliyofanyika kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar juzi. Tanzania iliwafunga Guinea bao 1-0 na kutwaa taji hilo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Clara Luvanga arejea Twiga Stars

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Al Nassir FC ya Saudi Arabia, Clara Luvanga, ameitwa katika kikosi cha Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), kilichoingia kambini jana kujiandaa na mechi mbili za kirafiki za kimataifa, imefahamika.

Twiga Stars itacheza mechi hizo za kirafiki baadaye mwezi huu kwa ajili ya kujiandaa na Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (WAFCON), zitakazochezwa hivi karibuni.

Awali fainali za WAFCON zilipangwa kufanyika Julai, mwaka huu nchini Morocco, lakini zimehamishwa hadi hapo itakavyotangazwa tena.

Ofisa Habari wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, alisema mazungumzo kuhusiana na timu itakayocheza dhidi ya Twiga Stars yanaendelea na yatawekwa wazi baada ya kukamilika.

Kikosi kamili cha Twiga Stars ni Najat Abbas, Lidya Maximilian, Christer Bahera, Janeth Pangamwene, Maimuna Kaimu, Joyce Lema, Jamila Rajabu, Winifrida Gerald na Stumai Abdallah (JKT Queens), Asha Mrisho (Amani Queens), Enekia Kasongo (Easter Flames, Saudi Arabia).

Wengine ni Julietha Singano (Juares, Mexico), Suzan Adam Tuthankhamu, Misri), Diana Lucas (Ame D.F.K, Uturuki), Oppa Clement (Besikta, Uturuki), Aisha Masaka (BK Häcken. Sweden), Aisha Mnuka (Simba Queens) na Asha Ramadhan wa Yanga Princess.

## Mnunka: Nilifikiria kufunga mabao 25


**Na Saada Akida**

WAKATI Simba Queens wanahitaji pointi moja ili kujihakikisha ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania msimu huu, kinara wa kupachika mabao, mshambuliaji wa timu hiyo, Aisha Mnunka, amesema malengo yake makuu ni kuona wanatwaa taji la msimu huu.

Mnuka na Stumai Abdallah wa JKT Queens, wote wakiwa Watanzania wanachuana vikali kuwania kiatu cha dhahabu.

Straika huyo wa Simba Queens akiwa ametikisa nyavu mara 18 wakati Stumai amefunga magoli 16.

"Nikipata nafasi natumia kwa sababu nataka timu yangu ishinde, lakini lengo langu la pili ni kuwa mfungaji bora, mwanzoni malengo yangu yalikuwa kufunga mabao 25, naona natakiwa kuzidisha ili kuwa mfungaji bora," alisema Mnunka.



Katika msimamo wa ligi hiyo itakayorejea tena dimbani kuanzia Juni 7, mwaka, Simba Queens inaongoza ikiwa na pointi 43 na JKT Queens, mabingwa watetezi wakiwa nafasi ya pili na pointi 34 kibindoni.

## Makocha 412 riadha wapatiwa mafunzo

**Na Shufaa Lyimo**

MAKOCHA 412 kutoka mikoa mbalimbali nchini wamepatiwa mafunzo rasmi ya mchezo wa riadha, imeelezwa.

Ofisa wa Michezo wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Charles Maguzu, amesema baraza limeamua kufanya programu hiyo baada ya kugundua idadi kuwa ya makocha walikuwa wanafundisha mchezo huo bila kuwa na ufahamu rasmi.

"Tumefanya programu hiyo baada ya kugundua walimu wengi wanafundisha riadha hali ya kuwa hawana taaluma ya mchezo wanaousimamia," alisema Maguzu.

Aliongeza programu hiyo imewajengea uwezo makocha hao kwenda kuwaandaa wachezaji chipukizi lakini pia wamebaini walimu hao hawana vifaa na wamekuwa na changamoto ya kukosa ruhusa ya kuhudhuria mafunzo mbalimbali.

"Ili kupata wachezaji kwenda kushiriki mashindano ya kimataifa ni mafanikio makubwa na hiyo inatokana na juhudi zinazofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Samia Suluhu Hassan," Maguzu alisema.

# Michezo

Jumapili Mei 26, 2024

Nipashe



## Ten Hag: Sina uhakika kubaki

UKURASA 22




Nahodha wa Yanga Bakari Mwamnyeto na kipa Djigui Diarra wakiwa wamenyanyua Kombe la ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu wa mwaka 2023/24 waliloka-bidhiwa rasmi baada ya mechi ya ligi dhidi ya Tabora United iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana. **PICHA: MTANDAO**

# AZIZ KI ANOGESHA SHEREHE

## Vita yake na Fei Toto yakolea, Mtibwa Sugar yashuka rasmi...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

BAO lililofungwa na mshambuliaji wa Yanga, Stephanie Aziz Ki katika ushindi wa magoli 3-0 dhidi ya Tabora United liliwanyanyua mashabiki wa timu hiyo na kunogesha sherehe maalumu ya kukabidhiwa kikombe iliyofanyika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana.

Mashabiki wa Yanga walionekana kupooza kutokana na mshambuliaji wao huyo nyota kupitwa idadi ya magoli na Feisal Salum 'Fei Toto' wa Azam FC, ambao jana kila mmoja alifikisha magoli 18 na kuifanya vita ya kuwania kiatu cha dhahabu kuendelea kuwa ngumu.

Hata hivyo watani wa Yanga, Simba ambao jana walipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya KMC, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid Jijini Arusha huenda wakakosa tiketi ya kushiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao kutokana na Azam kujiimarisha katika nafasi ya pili.

**Hii ni baada ya ushindi wa mabao 5-1 iliyoupata Azam FC, iliyokuwa nyumbani kwenye Uwanja wa Azam Complex, dhidi ya Kagera Sugar.**

Wakati hayo yakiendelea, timu ya Mtibwa Sugar imeshuka daraja rasmi baada ya kucheza Ligi Kuu kwa misimu 28, ilipopanda mwaka 1996, ilipokubali kipigo cha mabao 3-2 kutoka kwa Mashujaa FC, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma.

Mabao mengine ya Yanga katika mechi ya jana yalifungwa na Joseph Guede dakika ya 19 huku Maxi Mzengeli akipachika la pili dakika ya 48 wakati Aziz Ki aliyefunga dakika za majeruhi alimfikia Fei Toto ambaye jana alipachika mabao mawili.

Magoli mengine ya Azam FC katika mchezo wa jana yalifungwa na Kipre Junior, Idd Nado na Gibril Sillah, ikifikisha pointi 66 na mabao 61.

Simba, ilipata ushindi wa bao 1-0 lililofungwa na Saido Ntibazonkiza dakika ya pili, lakini uliendelea kuibakisha nafasi ya tatu kwa pointi 66 na bao 57.

Hatima ya timu moja kati ya Simba au Azam kucheza Ligi ya Mabingwa sasa itaamuliwa katika mechi ya mwisho, Mei 28, wakati Wekundu wa Masimbazi watacheza dhidi ya JKT Tanzania na Azam itakuwa Nyankumbu, ikicheza dhidi ya Geita Gold.

Ikiwa kwenye uwanja wake wa nyumbani, Lake Tanganyika, Mashujaa FC imeichapa Mtibwa Sugar mabao 3-0, mawili yakiwekwa wavuni na Reliants Lusajo dakika ya tatu na 26, Munhir Viai alitupia la tatu dakika ya 32, bao la kufutia machozi la Wakatamiwa hao yakifungwa na Seif Karihe, ambayo hayakutosha kuwabakisha Ligi Kuu, kwani hata kama ikishinda itafikisha pointi 24, ambazo zimeshapitwa na Geita Gold ambayo ina pointi 25, ikisubiri hatma yake dhidi ya Azam FC.

Coastal Union imeonyesha nia yake ya kucheza michuano ya kimataifa msimu ujao ilipolazimisha suluhu dhidi ya JKT Tanzania, na kufikisha pointi 42, ikiwa nafasi ya nne ya msimamo.

Pazia la Ligi Kuu Bara litafungwa rasmi keshokutwa kwa mabingwa kucheza dhidi ya Prisons, Simba yenyewe itawaalika JKT Tanzania, Coastal Union dhidi ya KMC, Dodoma Jiji itawafuata Mashujaa wakati Ihefu itawaalika Mtibwa Sugar na Namungo itakabili Tabora United.

Mechi nyingine itakuwa ni kati ya Geita Gold FC dhidi ya Azam na Singida Fountain Gate itawakaribisha Kagera Sugar.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042